# IMAM ALI
# NA
# MAMBO YA UMMA

الإمام على عليه السلام وقضايا الأمة

**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hassan Musa as-Saffar

**Kimetarjumiwa na:**
Abdul-Karim Juma Nkusui

**Kimehaririwa na:**
Alhaji Hemedi Lubumba

**Kimepitiwa na:**
Mbaraka A. Tila

# ترجمة

# الإمام على عليه السلام وقضايا الأمة

## تأليف


## الشيخ حسن الصفار


## من اللغة العربية إلى اللغة السواحلية

©**Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN:** 978 - 9987 – 17 – 048 – 7

**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hassan Musa as-Safar

**Kimetarjumiwa na:**
Abdul Karim Juma Nkusui
**Barua pepe:** abdulkarimjuma@yahoo.com

**Kimehaririwa na:**
**Alhaji Hemedi Lubumba**

**Kimepitiwa na:**
Mbaraka A. Tila

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Januari, 2014
**Nakala:** 2000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com
**Tovuti:** www.ibn-tv-com
**Katika mtandao:** www.alitrah.info

# YALIYOMO

Neno la Mchapishaji ........................................................................01

Utangulizi............................................................................................03

Imam Ali na Umoja wa Ummah ...................................................06

Upande Wowote Hauna Haki ya Kulazimisha
Rai yake Katika Jamii ......................................................................30

Imam Ali ni Kiongozi wa Urekebishaji ........................................33

Ima Urekebishaji wa Jumla au Mlipuko wa Ndani.......................54

Kuendeleza Ubinadamu Katika Zama za Imam Ali .....................57

Ndio, kwa Kuanzisha Vyama vya Kiraia vya Kijamii
Katika Nchi yetu ...........................................................................76

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako asili yake ni kitabu kilichoandikwa kwa lugha ya Kiarabu cha Sheikh Hassan Musa as-Saffar.

Kitabu hiki ni mwendelezo wa mihadhara inayotolewa na Sheikh wetu huyu kwa ajili ya kuelimisha Umma.

Katika mhadhara huu ambao ulifanyika mjini Qataf nchini Hijaz (Saudia), Sheikh alimzungumzia Imam Ali (a.s.) kama kiongozi wa Umma, kiongozi wa urekebishaji, kuendeleza ubinadamu, na alizungumzia pia kwamba upande wowote hauna haki ya kulazimisha rai yake kwa jamii.

Kama wote tujuavyo, Imam Ali (a.s.) alikuwa kiongozi mwadilifu na anayekubaliwa si kwa Waislamu tu bali na jamii zote za wanadamu. Na kwa nini isiwe hivyo wakati amelelewa na mtu mtukufu mbora wa viumbe naye si mwingine bali ni Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), ambaye alimpa sifa ya mlango wa elimu yake yeye mwenyewe (s.a.w.w.) akiwa ni mji ya elimu.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana hususan wakati huu ambapo maadili ya uongozi yameporomoka na ufisadi umetawala kila mahali ulimwenguni. Hivyo, tukaona tukichapishe kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili ili ujumbe huu ufike kwa wasomaji wetu wa Kiswahili ambalo ndio lengo la taasisi yetu hii ya Al-Itrah Foundation.

Tunamshukuru Ndugu yetu Sheikh Abdul-Karim Juma Nkusui kwa kazi kubwa aliyoifanya kukitarjumi kitabu hiki kwa lugha

ya Kiswahili na wengine wote waliomsaidia kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah Mwenye kujazi awalipe wote malipo mema ya hapa duniani na huko Akhera pia.

**Mchapishajji**
**Al-itrah Foundation**

# UTANGULIZI

بسم الله الرحمن الرحيم

**Kwa Jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu**

Sifa zote njema anastahiki Mola wa viumbe. Eee Mwenyezi Mungu mswalie Muhammad na kizazi cha Muhammad kama ulivyomswalia Ibrahim na kizazi cha Ibrahim. Na Mbariki Muhammad na kizazi cha Muhammad kama ulivyombariki Ibrahim na kizazi cha Ibrahim, hakika Wewe ni Mwenye kuhimidiwa Mtukufu.

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

**لَا خَيْرَ فِي كَثِيرٍ مِنْ نَجْوَاهُمْ إِلَّا مَنْ أَمَرَ بِصَدَقَةٍ أَوْ مَعْرُوفٍ أَوْ إِصْلَاحٍ بَيْنَ النَّاسِ ۚ وَمَنْ يَفْعَلْ ذَٰلِكَ ابْتِغَاءَ مَرْضَاتِ اللَّهِ فَسَوْفَ نُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا**

**"Hakuna kheri katika siri zao nyingi, ila mwenye kuamrisha sadaka au wema au kusuluhisha watu. Na mwenye kufanya hayo kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu, basi tutampa ujira mkubwa." (Surat Nisaai: 114)**.

Ni uzuri ulioje kumzungumzia Ali bin Abu Talib (a.s.)?

Na ni umbali ulioje wa upeo wa shakhisiya yake tukufu?

Na ni haja ilioje katika zama hizi, Ummah kuisoma sira yake tukufu, mfumo wake mnyoofu na rai zake zenye uongofu?

Hakika Ummah unahitaji ushujaa wa Ali bin Abu Talib (a.s.), nao unakabiliana na kiburi cha ubeberu wa kiulimwengu, na utawala wa wageni katika ardhi nyingi za Kiislamu. Inahitajika hekima ya Ali na subira yake katika kukabiliana na ikhtilafu za ndani kwa ajili ya kuhifadhi umoja na kuhami usalama wa kijamii. Unahitajika mfumo wake katika urekebishaji wa kisiasa, kupiga vita ufisadi na kuondoa ubaguzi baina ya watu, ili kanuni itawale, na uadilifu na usawa utekelezwe. Unahitajika uoni wake na umadhubuti wake katika kupambana na Makhawariji waasisi wa fikra za kukufurisha Waislamu, ubabe na ugaidi. Ndiyo, Ummah unamhitaji Ali (a.s.) katika kila nyanja ya sira yake, upeo wa mfumo wake na fikra yake.

Kitabu hiki kilichopo mbele ya msomaji mpendwa ni jaribio dogo la kuchukua mwangaza kutoka katika mionzi ya sira ya Ali na fikra yake, katika kutatua baadhi ya mambo ya hali ya Ummah wa leo. Asili yake ni muhadhara wa wazi nilioutoa katika ratiba iliyoandaliwa na kitengo cha Imamu Hasan (as) huko Qatif, katika kuhuisha kumbukumbu ya kifo cha Imam Ali (as), semina iliyofanyika katika usiku wa kumi na tisa, ishirini na ishirini na moja katika mwezi mtukufu wa Ramadhani 1427 Hijiria. Ilikuwa ni ratiba kubwa na nzuri iliyotokana na juhudi za ndugu watukufu wa kitengo hiki, ambapo waliandaa ukumbi mkubwa na wakatayarisha ratiba mbalimbali zenye manufaa, na wahudhuriaji walikuwa wengi wanaume kwa wanawake.

Na baadhi ya ndugu wapendwa walifanya kazi ya kuandika mihadhara hiyo mitatu na wakaipitia, kuisahihisha, kuipanga na kuandika upya baadhi ya vipengele vyake, kisha kitengo cha Imamu

Hasan (as) kimeichapisha na kuisambaza ndani ya kijitabu hiki kidogo chini ya anwani **Imam Ali na Mambo ya Ummah**. Mola awalipe malipo mema na tunawaombea mafanikio zaidi katika kuitumikia dini na jamii.

**Hasan Musa as Safar - Qatif,**
**5 Sha'aban 1428 Hijiria,**
**sawa na 18 Agosti 2008**

# IMAMU ALI (AS) NA UMOJA WA UMMAH

Katika kusoma kwetu shakhsiya ya Imam Ali bin Abu Talib (as) ni wajibu tujitahidi kurejesha fahamu zetu kwake, na hiyo ni kutokana na uelewa wa wakati wetu na mazingira yetu, *Ali bin Abu Talib* ni kitabu chenye madhumuni ya kina, kinajirejesha upya kila zama na katika kila mazingira, na kila kizazi kinaweza kusoma kitabu hiki na kuchukua kutoka kwake kile kinachofaa mazingira yake na kurekebisha mambo yake. Na katika kusoma kwetu inapasa tusiwe mateka wa usomaji wa waliotangulia, kila kizazi kinamsoma Ali kulingana na uelewa wake na mazingira yake. Kuna anayemsoma Ali (as) kama muujiza wa ghaibu, kama mawalii wengine ambao Mwenyezi Mungu Mtukufu anawapa upeo wa kuvuka hali ya kawaida na kuvuka yaliyozoeleka, pindi hekima yake (swt) na matakwa yake yanapohitaji hivyo, lakini hali hiyo ni ya nadra sana, kwa sababu Ali, Maimamu wengine na Manabii - amani iwe juu yao wote – wote asili yao ni wanadamu, Mwenyezi Mungu anasema:

قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِثْلُكُمْ يُوحَى إِلَيَّ أَنَّمَا إِلَ هُكُمْ إِلَ هٌ وَاحِدٌ

**“Sema: hakika mimi ni binadamu kama nyinyi tu, nimeletewa wahyi kwamba Mungu Wenu ni Mungu Mmoja.” (Surat al-Kahfi: 110)**.

Asili katika maisha yao ni hali ya kawaida ya kibinadamu na hautokei muujiza au karama isipokuwa ujumbe unapohitaji kufanya hivyo.

## KUTILIA MKAZO HALI YA KIMUUJIZA:

Hakika baadhi yetu hutaka kutoa kisingizio cha kutowafuata Manabii na Maimam (as), hivyo huwatazama katika hali isiyokuwa ya kibinadamu ili wapate udhuru mbele ya nafsi zao na mbele ya watu wengine wa kutowafuata wao (as), kwani haiwezekani kulinganisha baina ya hali ya kibinadamu na nyingine isiyokuwa ya kibinadamu.

Zaidi ya hapo ni yale mawazo tuliyorithishana kuhusu binadamu shujaa, ambapo tunamjengea sura katika akili zetu kana kwamba yeye sio mtu wa kawaida, nayo ndio dhana ya binadamu wa kawaida, na kwa ajili hiyo ndio maana tunaona filamu za katuni zinazoelekezwa kwa watoto wetu, mara zote zinamuonesha shujaa katika umbo la binadamu asiyekuwa wakawaida, mwenye nguvu kubwa ya kimwili, na mwenye uwezo usiokuwa wa kawaida. Hata kama hatupingi kutokea kwa miujiza na karama kwa Manabii na mawalii kwa idhini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na sio kwa uwezo wao binafsi, kama inavyosimulia Qur'ani Tukufu juu ya miujiza ya Manabii kama vile Nabii wa Mwenyezi Mungu Isa (as) katika kauli yake (swt):

أَنِّي أَخْلُقُ لَكُمْ مِنَ الطِّينِ كَهَيْئَةِ الطَّيْرِ فَأَنْفُخُ فِيهِ فَيَكُونُ طَيْرًا بِإِذْنِ اللَّهِ وَأُبْرِئُ الْأَكْمَهَ وَالْأَبْرَصَ وَأُحْيِي الْمَوْتَى بِإِذْنِ اللَّهِ وَأُنَبِّئُكُمْ بِمَا تَأْكُلُونَ وَمَا تَدَّخِرُونَ فِي بُيُوتِكُمْ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَةً لَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ

**"Hakika mimi nitawafanyia kama namna ya ndege katika udongo; kisha nimpulizie awe ndege kwa idhini ya Mwenyezi Mungu na niwaponye vipofu na wenye mbalanga. Niwafufue wafu kwa idhini**

**ya Mwenyezi Mungu. Na niwaambie mnavyovila na mtakavyoweka akiba. Hakika katika haya ipo ishara kwenu mkiwa ni wenye kuamini." (Surat Imran: 49)**.

Na kama ilivyopokewa katika Qur'ani Tukufu karama za Bibi Mariam binti Imran:

كُلَّمَا دَخَلَ عَلَيْهَا زَكَرِيَّا الْمِحْرَابَ وَجَدَ عِنْدَهَا رِزْقًا قَالَ يَا مَرْيَمُ أَنَّى لَكِ هَ ذَا قَالَتْ هُوَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ

**"Kila mara Zakariya alipoingia Mihrab hukuta vyakula. Akasema: Ewe Maryam, unatoa wapi hivi. Akasema: Vinatoka kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu humruzuku amtakaye bila hesabu." (Surat Imran: 37)**.

Na kwa kuongezea ni miujiza ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) inayopokewa na Waislamu, ikiwa ni pamoja na karama za baadhi ya Masahaba, Maimamu na Mawalii zinazopokewa na makundi mbalimbali katika Ummah. Pamoja na yote hayo, lakini miujiza ya Manabii na karama za Mawalii kwa hakika hufanyika kwa idhini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika hali ya kipekee na ya nadra, pale hekima na matakwa yake (swt) yanapohitajia hivyo, na sio hali ya daima ya mara kwa mara, na sio kwa amri ya Nabii au Walii, na kwa sababu hiyo Nabii Muhammad (saww) alikataa maombi ya washirikina walipomuomba kuleta muujiza, kama vile kutoa chemchem ya maji yenye kutiririka toka ardhini, au aangushe juu yao kipande cha mbingu au atengeneze nyumba ya dhahabu, akawajibu kama anavyosema Mwenyezi Mungu:

أَوْ يَكُونَ لَكَ بَيْتٌ مِنْ زُخْرُفٍ أَوْ تَرْقَى فِي السَّمَاءِ وَلَنْ نُؤْمِنَ لِرُقِيِّكَ حَتَّى تُنَزِّلَ عَلَيْنَا كِتَابًا نَقْرَؤُهُ ۗ قُلْ سُبْحَانَ رَبِّي هَلْ كُنْتُ إِلَّا بَشَرًا رَسُولًا

**"Au uwe na nyumba ya dhahabu au upae mbinguni. Na hatutaamini kupaa kwako mpaka ututeremshie Kitabu tukisome. Sema: ametakasika Mola Wangu! Kwani mimi ni nani, isipokuwa ni mwanadamu Mtume?" (Surat Israa: 93)**.

Isipokuwa kuna aina ya kutia chumvi na kupita kiasi katika hazina za makundi na madhehebu, kuhusu miujiza na karama za Manabii, Maimamu na Mawalii, na wala haisihi kukubali isipokuwa ile iliyokuja kwa sanadi inayokubalika na isiyokhalifu chochote kati ya misingi ya Kitabu na Sunnah.

## KUTILIA MKAZO UPANDE WA HUZUNI:

Kuna baadhi ya wenye kumpenda Ali (as) wamemsoma kama kielelezo cha hali ya huzuni, na huu ni upande wenye uhalisia katika maisha ya Imamu Ali (as), kwani Imamu Ali (as) alikabiliwa na dhulma nyingi katika maisha yake, na hata baada ya kufariki kwake, lakini uhalisia wa juhudi zake na jihadi yake ni mkubwa zaidi kuliko udhibiti wa kona ya huzuni na dhulma. Hakika baadhi yetu wanaelezea kwamba karibu nusu ya maisha ya Amirul-Muuminina (as) yalikuwa ni ya kujitenga na upweke, na kwamba hakufanya kazi yoyote ya Ummah baada ya kufariki Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), hadi alipochukua ukhalifa, yaani miaka ishirini na tano (muda wa robo karne), na hakufanya chochote wala jukumu lolote!

Hakika anayeng'ang'ania kwamba Ali alikuwa amekaa katika nyumba yake amejitenga kwa huzuni na majonzi ya kupokonywa ukhalifa, na wala hakuhisi jukumu lolote kuhusu hali ya Ummah, bila shaka mtu huyo ameghafilika kwamba madai haya hayafanani na fikra ya Imam Ali (as), mfumo wake na maelekezo yake (as), wala hayaafikiani na yaliyoandikwa na historia kuhusu nafasi yake na misimamo yake katika hatua hiyo. Imamu Ali (as) alikuwa anawaambia watu: "Mcheni Mwenyezi Mungu katika waja wake na nchi yake hakika nyinyi ni wenye kuulizwa hata kuhusu sehemu na wanyama."[1] Hakika ukhalifa kwa Imam Ali (as) haukuwa ni jambo la msingi kiasi kwamba adumaze maisha yake kwa kuukosa, kwa sababu kutaka vyeo kunaweza kuzishughulisha nafsi zetu sisi. Tunapokosa vyeo hivyo au nafasi hizo tunahisi kana kwamba tumekosa nafasi yetu katika maisha haya, kwa hiyo utakuta mmoja wetu anahuzunika na kunyong'onyea kwa kukosa kwake cheo alichokuwa anakitarajia au nafasi aliyokuwa nayo.

Lakini Ali bin Abu Talib hakuwa hivyo, kwa sababu ukhalifa hata siku moja haukuwa ni lengo la matarajio yake. Anasema Abdillah bin Abbas: "Niliingia kwa Amirul-Muuminina (as) huko Dhiy Qaari, naye akiwa anashona kiatu chake, akaniambia: 'Nini thamani ya kiatu hiki?' Nikasema: Hakina thamani. Akasema (as): 'Wallahi hakika nakipenda zaidi kuliko uongozi wenu huu, isipokuwa kama ni kusimamisha haki au kuondoa batili.'"[2] Hakika sisi tunapojua mtazamo wa Imamu Ali (as) kuhusu thamani ya vyeo hivi hatuwezi kuyafunga maisha yake ya kipindi cha baina ya kufariki Mtume (saww) na kuchukua kwake ukhalifa, kwamba ni kipindi cha maisha ya kujitenga na masikitiko. Lakini baadhi ya vizazi kwa kuwa vilikuwa vinaishi kwa kujitenga, kunyong'onyea

[1] Sharifu Ridhaa: Katika *Nahjul-Balaghah*, Kimehakikiwa na *Muasasatu Nahjul-Balaghah*, Chapa ya 3, 1316 Hijiria, Hotuba ya 166.
[2] *Nahjul-Balaghah*, Hotuba namba 33.

na kubaki nyuma, walijaribu kutoa visingizio vya kuhalalisha na kutetea hali hii, lakini hakika tunaposoma kwa maudhui tunakuta kwamba Ali bin Abu Talib (as) hakuacha kazi yake ya ujumbe hata siku moja, bali daima alikuwa anabeba jukumu katika ujumbe na Ummah.

Na katika nukta hii ni juu yetu tuwe waadilifu katika haki ya hali yetu na historia yetu, na hiyo ni kwa sababu katika miongo mingi ya historia Mashia wameendelea kukandamizwa sana. Wengi kati yao wamelazimishwa kujitenga na kudumaa, na pengine hali hii ya kijamii waliifikia kwa sababu ya baadhi ya mazingira ambayo yalikuwa na nafasi katika kuwafikisha hapo, na yaliyowazuia kufunguka hadi ndani ya jamii za Waislamu wengine. Na kwa sababu hiyo utakuta mengi kati ya mawazo haya na maelekezo haya yanatilia mkazo upande wa huzuni katika maisha ya Imamu Ali (as) na Maimamu wengine (as) ili kuendana na hali ya jumla ambayo walikuwa wanaishi nayo Mashia wengi.

Hakika kusoma maisha ya Imam Ali (as) kwa usomaji wa kuiga kunaifunga nafasi ya Ali (as) katika upande wa huzuni tu baada ya kufariki Mtume (saww), na kunatilia mkazo nafasi yake katika uhai wa Mtume (saww) na wakati wa kuchukua kwake ukhalifa tu, na usomaji huu hautupatii sura halisi ya jukumu alilolifanya Imam (as), na hususan baada ya kufariki Mtume (saww). Hakika jukumu ambalo alilifanya Imam Ali (as) baada ya kufariki Mtume (saww) ni kati ya muonekano ulio muhimu sana wa ikhilasi yake kwa maslahi ya dini na Ummah, utukufu wa nafsi yake na kutokuathirika kwake na hisia na maslahi binafsi. Imam (as) amehifadhi umoja wa Ummah katika mazingira hatari na amechunga hali ya Uislamu ambayo ilikuwa inahitaji rai zake za sawa na maarifa yake ya kina katika kufahamu dini na utekelezaji wa hukumu zake.

# DHANA YA UMOJA:

Hakika dhana ya umoja inaweza kukanganya katika akili za watu, kana kwamba umoja ni kufuta sifa maalumu za upande mmoja kwa ajili ya upande mwingine au upande mmoja kuyeyuka ndani ya upande mwingine, au kundi hili kuacha jambo ambalo wana yakini nalo kwa ajili ya kundi jingine. Ufahamu huu wa kimakosa juu ya umoja ndio ambao umeufanya uwe ni mazigaziga usiowezekana kupatikana katika hali ya Waislamu, kwa sababu baadhi wanafikiria kwamba umoja ni kuafikiana kikamilifu katika kila kipengele cha itikadi, sharia, rai na mwelekeo. Na hii inapingana na tabia ya binadamu, maadamu wana rai na maslahi tofauti lazima ikhitilafu zitapatikana hata ndani ya familia moja na jamii moja. Hakika tunapofungamanisha baina ya umoja na baina ya kuafikiana kila kitu, hakika kwa hilo tunakuwa tunatafuta mazigaziga ya umoja ambao kamwe hautapatikana. Ama tunapotazama umoja kwa msingi wa kipenyo cha sehemu za ushirikiano, maslahi ya Ummah na kuungana chini ya msingi ambao unatukusanya sote, unaheshimu haki za wote na kutoa fursa sawa ya kutoa mawazo, hakika umoja huu unaweza kupatikana.

Na mataifa mengine yameshaupata, hawa ni Wamarekani, watu wa Ulaya, Wajapani, Wamalezia, Wahindi na mataifa mengine, hawa wamefikia daraja ya juu ya umoja bila kufuta sifa maalum za baadhi yao au bila ya kuwa na dhulma au bila kuwepo uonevu dhidi ya upande mmoja, au upande mmoja kuukandamiza upande mwingine, na hili ni jambo la kawaida ambalo linapasa liwe, na sisi tunapozungumzia umoja ni kwa dhana hii. Na tunaposoma sira ya Imamu Ali (as) baada ya kuondoka Mtume (saww), tunaona tofauti iliyojitokeza kuhusu kuchukua nafasi ya ukhalifa na uongozi wa Ummah, na Imamu anaona yeye ndio mwenye haki hii na kwamba yeye anasta-

hiki zaidi cheo hiki, lakini hakufanya hiyo ndio sababu ya ugomvi na mgongano, bali alilinda rai yake bila ya kuwatenga wapinzani wake, na bila kufanya ubakhili wa kuwapa nasaha yake, na hakuzembea kutoa juhudi zake katika kutumikia dola na Ummah.

Misimamo hii ya kiujumbe ya Imam Ali (as) baadhi ya Sunni na Shia hawakuifahamu, ambapo kundi limefasiri kiapo cha utii cha Imam Ali kwa Makhalifa na kushirikiana pamoja nao, kwamba ni dalili ya Imam kuacha rai yake katika haki yake ya ukhalifa, wakati ambapo kundi jingine limepinga uhusiano wowote mzuri baina ya Imam Ali na Makhalifa. Rai zote mbili hazina uadilifu, Imam Ali alilinda rai yake, isipokuwa alitanguliza maslahi ya Ummah kwa ajili ya Ummah, kwa kuhifadhi umoja wake na kusahihisha misimamo ya viongozi wake.

# MWELEKEO WA UMOJA:

Na kwa kuelewa sira ya Amirul-Muuminina (as) na kwa kuangalia mtazamo wake tunaweza kugawa mazungumzo ya umoja katika mielekeo mitatu:

## KWANZA: UMOJA WA KIJAMII:

Sisi kama jamii tunaishi katika sehemu moja, ndani ya duara la madrasa ya Ahlulbayt (as), tunawakilisha hali ya kijamii, tunakusanywa pamoja na utamaduni mmoja unaokaribiana, tunaishi kwa huzuni na matarajio mamoja. Tumo ndani ya utambulisho mmoja wa kidini, na kwa ajili ya kuhifadhi utambulisho huu na kufikia katika kuendeleza

jamii zetu na kuziboresha, ni wajibu kuwepo na ushirikiano baina ya nguvu za jamii na harakati zake. Na hii haimaanishi kuafikiana katika rai zote na fikra zote, kama wanavyodhani baadhi yetu hivyo, kwa mfano wanadhani ni lazima wanajamii wote wamfuate Marjaa mmoja, na kwamba kulingania umoja ni kutokuwa na Marjaa wengi. Au utendaji wetu katika baadhi ya harakati uwe ni mmoja na kwa namna na njia moja. Na umoja unakuwa kana kwamba ni kulingania kwenye kukhalifu mazingira ya kibinadamu. Bila shaka sisi tunapolingania kwenye umoja wa kijamii, hakika tunalingania kwenye kuunganisha misimamo ya Ummah katika yale ambayo kikawaida yanaathiri katika jamii kwa ujumla, ikiwa ni pamoja na kuheshimu uhuru wa kutoa mawazo, kwa sababu kuwepo na rai nyingi na mielekeo mingi ni jambo la kawaida na ni hali njema katika jamii yoyote, kwani inaelezea utajiri wa uhuru wa kutoa rai na fikra.

Na mukabala na tofauti hizi za rai na fikra kuna maslahi ya pamoja yanayotukusanya sote pamoja, yanayotufunika sote katika paa moja, na haya ndio tunayopasa kuyatafuta na kuyakusanyikia. Na alhamdulillahi kwamba jamii yetu imeanza kuyavuka matatizo mengi ambayo yalikuwepo katika nyakati fulani, tofauti za madrasa za kifiqhi na kifikra ndani ya jamii moja ya Kishia zilikuwa ni sababu za mzozo na utengano katika nyakati fulani, baina ya *Usuliyiina*, *Ikhibariyiina* na *Shaikhiy*, lakini hivi sasa tofauti hizo si sababu tena za mizozo na ikhitilafu isipokuwa katika mabaki machache na yasiyoathiri.

Na kuna wakati kulikuwa na mzozo wa kimarjaiyyah. Kulikuwa na kundi lina kasumba na Marjaa fulani, na jingine lina kasumba na Marjaa mwingine, na wala haliruhusu kumfuata Marjaa wa kundi jingine. Mara inakuja fatwa huku ikiunga mkono Marjaa fulani na mukabala na fatwa hiyo inaletwa fatwa nyingine dhidi ya Marjaa yule, katika hali ya mzozo na malumbano ya kimaneno na ya kijamii.

Kama ambavyo katika baadhi ya hatua kulikuwa na tofauti dhahiri katika mielekeo na rai za kisiasa ambazo baadhi yake zilisababisha aina ya mizozo na ugomvi baina ya wafuasi wa mwelekeo huu na ule. Lakini sisi hivi sasa tunaishi kwa ukaribu katika mielekeo ya kisiasa na hakuna tena tofauti kubwa, na haijabakia isipokuwa hali ya ushindani wa kawaida baina ya mielekeo, makundi na watu, na hii ni hali ya kawaida maadamu tu inahukumiwa kwa tabia njema. Na yaliyotokea katika harakati za uchaguzi wa Manispaa wa mwaka 1426 Hijiria katika nchi yetu, ikiwa ni pamoja na ushindani uliokuwepo baina ya mgombea mmoja na mwingine au baina ya kundi moja na jingine, ni hali ya kawaida ambayo hutokea katika kila jamii.

Na maadamu tumeondokana na mzozo kwa msingi wa ufuasi wa madrasa za *Usuliyiina*, *Ikhibariyiina* na *Shaikhiy*, na vile vile kwa msingi wa ufuasi wa *marjaiyyah*, na haikubaki kwetu mzozo mkali kwa msingi wa kutofautiana rai na mielekeo ya kisiasa. Hatua hii ni ya kusonga mbele katika njia ya kufanikisha umoja wa kijamii, maadamu tu haijabaki mbele yetu isipokuwa maudhui ya ushindani baina ya makundi na jamaa au baina ya watu, na hili ni jambo la halali haliwezekani wala haipasi kulifuta. Hapa ni wajibu wetu kukumbuka umuhimu wa tabia ya ushindani, na tuitambue hali ya ushindani katika duara lake na maudhui yake.

Na katika mas'ala ya umoja wa kijamii inapasa kuashiria kwenye nukta tatu nazo ni:

**1. Kifua kipana wakati wa kutofautiana katika rai:**

Ni wajibu tuwe na subira wakati wa ikhitilafu za pembeni, kwani kuafikiana katika rai haitakiwi, bali ni juu yetu kuishindanisha rai na rai nyingine, kwa sababu baadhi yetu huwa wanakerwa na tofauti hata katika baadhi ya mas'ala ya matawi kama vile kuthibiti mwandamo wa mwezi katika siku hii au nyingine, au

wakati wa kuadhimisha mnasaba huu wa kidini katika usiku huu au usiku mwingine. Ni sahihi kwamba kuafikiana rai katika hayo kunahifadhi umoja wa kijamii, lakini maafikiano haya hayawezi kuwa na nguvu ya kuondoa tofauti za ukinaifu unaohusu maudhui yanayofungamana na upande wa kiibada kama vile Saumu kwa mfano. Hivyo basi inapasa kila mtu atekeleze kwa namna anayoona ni wajibu wake wa kisharia, na kutofautiana katika mambo mfano wa haya ni wajibu kupokewa kwa vifua vipana na wala mambo hayo yasiwe makubwa katika nafsi zetu. Lakini yanayosikitisha ni kwamba baadhi yetu bado wangali wanaishi katika ufinyu wa upeo, wanamaliza wakati wao kwa kuzungumzia kundi lile ambalo limefungua siku hii na lile ambalo limefunga. Inapasa tuivuke hali hii, sisi tuko dhidi ya wanaowakandamiza wengine katika jamii yetu, wale wanaotaka wanajamii wachukue rai yao na njia yao, vinginevyo wanawamiminia tuhuma na wanawatoa katika dini na madhehebu wale wanaowakhalifu.

Hakika sisi wakati ambao tunapinga wengine wasifanye ukandamizaji juu yetu, inakuwaje basi tunakubali kufanyiana ukandamizaji wenyewe kwa wenyewe? Hakika ni wajibu juu yetu kuimarisha hali ya ushindani mzuri, na wala tusiruhusu upande wowote kudai katika nafsi yake kwamba ni wenyewe peke yake ndio unaowakilisha dini, sharia na utawala. Hakuna yeyote mwenye hatimiliki ya kumiliki sharia, upande huu una rai na upande mwingine una rai nyingine, na hakuna yeyote anayeweza kudai kwamba yeye anawakilisha asili ambapo mwingine ni tawi, au kwamba anawakilisha dini ya haki na mwingine yuko nje ya dini. Tumeshavuka akili ya kutawaliwa, na vimemalizika vitendo hivi, na aina hii ya kuamiliana pamoja na wengine, hivi sasa watu wanafahamu jukumu lao na wanajiamini, na hivyo ni

wajibu wetu kuimarisha hali hii, vifua vyetu viwe vipana mbele ya baadhi ya ikhitilafu za ndani na tusizikuze katika nafsi zetu na tusiruhusu baadhi watengeneze kadhia wanayoitumia kuwagawa na kuwafarakisha watu.

## 2. Kueneza utamaduni wa usamehevu:

Viongozi wa jamii na wakuu wake wanabeba jukumu kubwa katika kueneza utamaduni wa usamehevu wa ndani baina ya makundi na mitazamo mbalimbali, na kuweka mpaka wa hali ya hamasa na uhamasishaji wa kupinga, kwa sababu sisi katika hatua hii ni wajibu wetu kutilia mkazo yale yanayotukusanya kama wafuasi wa Ahlulbayt (as) na tuliopo katika njia yao na madrasa yao, na ni wenye kutaraji uombezi wao, na inshaallah Mwenyezi Mungu Mtukufu atukusanye Siku ya Kiyama pamoja nao.

Katika nukta hii imepokewa riwaya nzuri kutoka kwa Imam as-Sadiq (as) akiwaeleza humo baadhi ya wafuasi wake, anasema: "Mna nini nyinyi?! Kwanini baadhi yenu wanajiepusha na wengine? Hakika waumini baadhi yao ni bora kuliko baadhi, na baadhi yenu ni wengi wa Swala kuliko baadhi, na baadhi yenu ni wenye uoni zaidi kuliko baadhi, na hizi ni daraja."[3]

Hakika kutofautiana rai na daraja za imani na viwango vya kufikiri haimaanishi kutengana, wala haihalalishi kutia chumvi katika mas'ala ya kulaumu. Ni wajibu wetu kukataa utamaduni wa uchochezi wa ndani na tusimame dhidi ya anayeueneza, na ni juu ya jamii ifike katika daraja ambayo itasimama dhidi ya kila upande wa kidini au wa kijamii unaotumia mbinu hizi za makosa.

[3] al-Majilisiy; Muhammad Baaqir katika *Biharul- An'war*, Juz. 66, uk. 168, Chapa ya 3 Daru Ihiyaai turathil- Islamiy, Beirut.

3. **Kujongea kwenye taasisi:**

Sisi hivi sasa tunaishi katika zama ambazo tunahitaji kazi za taasisi ambazo zinafanya kazi ya kujenga jamii kiutamaduni, kidini na kijamii, nazo ni zile zinazojulikana kama Taasisi za Kiraia za Kijamii, kwa mfano Jumuiya za Kujitolea, Klabu za Michezo, Mifuko ya Kujitolea ya Kuozesha, Mifuko ya Kusaidia Mayatima, Hafla za Ndoa za Pamoja, Vituo vya Kufundisha Qur'ani, na Klabu za Kawaida, bali ni wajibu wetu kubadili shughuli zetu zote kuwa za kitaasisi.

Msikiti ni wajibu uendeshwe na uongozi wa kamati iliyoridhiwa na watu wa sehemu husika, na hususan sisi tunaona baadhi ya vitongoji vimeshaunda kamati za vitongoji zilizochaguliwa na watu wa kitongoji husika, na tunatamani kila kitongoji kifuate fikira hii nzuri, hii ni hali ya kitaasisi nayo inatusaidia kushikamana na kushirikiana katika kulinda umoja wetu na kutumikia jamii yetu.

Na uzoefu wa kamati za vitongoji ni uzoefu mpya unaopendeza na inafaa yatekelezwe humo mas'ala ya ushindani mzuri katika msingi wa uwezo na vipaji. Na jambo hili lienee kwenye taasisi zetu zote za kijamii, ambapo inatakikana ziboreshwe kwa idara mpya na viongozi wapya, na ni wajibu kuchagua mgombea mwenye uwezo na mwingi zaidi wa harakati na uchangamfu. Zoezi hili litekelezwe katika Jumuiya za Kujitolea, Klabu za Michezo, na katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa na hata katika kuchagua Kamati za Uchumi na nyinginezo. Na katika yanayohusu Imam wa jamaa, katika upande wa kivitendo kila mtu miongoni mwetu ana uhuru wa kwenda kwa imam wa msikiti ambaye anapenda kuswali nyuma yake, aswali nyuma ya anayeamini uchamungu wake na anayehisi kwamba ananufaika na maelekezo yake bila kujali anatoka sehemu gani, anafuata Marjaa yupi, na anatoka katika familia gani, na kipimo kwake kinakuwa ni kipimo cha uwezo, na hiki ni kipimo ambacho kinakuza

na kuboresha jamii. Nukta hizi tatu ndizo zitakazotusaidia katika kuhifadhi umoja wetu wa kijamii.

## PILI: UMOJA WA KITAIFA:

Umoja wa Kitaifa ni maudhui nyeti sana na hatari, hususan katika wakati huu unaoupitia Ummah wa Kiislamu, Ummah ambao unatishiwa na hatari zinazogusa umoja wa wakazi wake na nchi zake. Hiyo ni kwa sababu Serikali ya Marekani inanyanyua kaulimbiu ya kutengeneza fujo na mizozo katika ukanda wa Mashariki ya Kati. Wao Wamarekani wanataka kugawanya kilichogawanywa na kutenganisha kilichotenganishwa, na kwa sababu hiyo ndio maana tunaona yanayotokea Iraki ili kuimarisha fujo na mzozo wa kutengenezwa ambao unatakiwa kuenezwa katika eneo lote (la Mashariki ya Kati).

Katika Palestina ambayo inakandamizwa na Uvamizi wa Kizayuni, huku wananchi wake wakikabiliwa na machungu na balaa, kila siku vinaongezeka vitendo vya mashambulizi, uharibifu wa nyumba, kuuwa viongozi, kuwatesa raia na kuwaweka jela. Pamoja na hayo bado kuna uhamasishaji ulio wazi wa vita vya ndani baina ya Wapalestina kutoka kwa Wamarekani, Mazayuni na washirika wao. Na bila shaka hali hiyo inatutanabahisha juu ya hatari, tunamuomba Mwenyezi Mungu awape tawfiki Wapalestina na awasaidie ili wavuke mtihani huu. Kama ambavyo juhudi za Serikali ya Marekani huko Lebanon za kuzuia maafikiano baina ya Walebanon hazifichikani kwa yeyote.

Na vivyo hivyo yanayotokea Somalia na Dafur Sudan, na wala sitaki hapa kuwabebesha lawama zote watu wa nje, kwani kama si mazingira mazuri na kuwepo mianya ndani yetu, na kama si nukta za udhaifu tulizonazo, basi maadui wasingepata fursa ya kuchochea

mfarakano na fitina ndani yetu, na hivyo ni juu yetu tuwe ni wenye tahadhari na wenye uelewa mzuri, kwa sababu kila panapopatikana vitisho dhidi ya maslahi ya wageni kunachochewa fitina upya. Alipoanguka Shaha wa Iran ambaye alikuwa anahami maslahi ya Wamagharibi na Wamarekani katika nchi hiyo, nchi hiyo ilikabiliwa na fujo za uchochezi wa kibaguzi na fitina za kimadhehebu. Na ilipopatikana nusura ya wapiganaji wa Hizbullahi huko Lebanon, zikatolewa fatwa za uchochezi, na ukatokea uchochezi upya wa fitina hizi za kimadhehebu.

Hii ni dalili kwamba kuna anayenufaika na fujo na mizozo hiyo, na ndiye anayeiunga mkono. Lakini katika asili kuna mazingira, mianya na nukta za udhaifu, hivyo ni juu yetu kuziondoa na kuzishughulikia, vinginevyo hakika maadui watazitumia ili kupanda fitina baina yetu. Hivyo ni wajibu tuwe makini katika kutilia mkazo mas'ala ya Umoja wa Kitaifa ndani ya nchi zetu, kwani nchi zetu zinalengwa. Na kuna mianya ambayo maadui wanaweza kuitumia katika kupenyeza sumu yao, hivyo ni lazima kuimarisha Umoja wa Kitaifa kwa kuzatiti na kutekeleza dhana ya utaifa, ili watu waishi kwa usawa katika haki zao na wajibu wao, na tusiruhusu – kwa kiwango cha kitaifa – utamaduni wa chuki na kuchochea ubaguzi na chuki baina ya kundi hili na kundi jingine.

Na maelekezo haya hayaelekezwi kwa kundi fulani tu, laahasha, mimbari zetu za kidini katika misikiti yetu na Husainiyya zetu, vile vile vyombo vya habari, (mitandao ya kijamii), (vyombo vya mawasiliano), khutuba katika misikiti na fatwa, ni wajibu kuwe na tahadhari katika yote haya, vyombo hivi visiwe silaha ya kutumikia mikakati ya fitina ambayo inatakiwa kuwashughulisha Waislamu na kuvuruga mambo yao. Na sisi wakati tunapotilia mkazo mas'ala ya umoja; hiyo ni kwa sababu fitina itakapotokea katika jamii, hakika haitabakisha wala haitasaza, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَاتَّقُوا فِتْنَةً لَا تُصِيبَنَّ الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْكُمْ خَاصَّةً وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ

**"Na jikingeni na fitna ambayo haitawasibu wale waliodhulumu miongoni mwenu peke yao, na jueni kuwa Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu." (Surat Anfal: 25)**.

Na katika mas'ala ya Umoja wa Kitaifa ni wajibu kutilia mkazo juu ya nukta muhimu, hiyo ni kwa sababu kila nchi kati ya nchi za ulimwengu kuna madhehebu na mielekeo mbalimbali, na ni kawaida kila kundi kati ya makundi haya kufanya shughuli zake na harakati zake makhususi na haiwezekani kuhesabu shughuli zake makhususi kuwa ni hali ya ubaguzi, maadamu tu linalinda mambo yake makhususi bila ya kugusa wengine. Na haikubaliwi kukataza watu kufanya mambo yao makhususi na mambo yao ya kimadhehebu kwa hoja ya kulinda umoja. Umoja haumaanishi kufuta mambo makhususi, na kuomba haki sio kuchochea ubaguzi na fujo, lakini inapasa kuomba haki kupitia mfumo wa kitaifa ambao unahifadhi umoja. Suala la kutoa rai na mawazo, na kuomba haki na kueleza matatizo katika vyombo vya habari na kupitia chaneli rasmi na kwa njia mbalimbali, ndani ya paa moja la nchi, ni suala linalotakiwa na wala halikhalifu msingi wa umoja, kwa sababu si zaidi ya kutoa rai na mawazo, kwani Umoja wa Kitaifa haumaanishi kuwepo na rai moja tu yenye kuenea na kutokuwa na haki kwa mwingine kutoa rai yake (au kuomba haki yake).

## TATU: UMOJA WA UMMAH:

Kwa hakika Umoja wa Ummah unapatikana kwa kutilia mkazo katika ushirikiano na juu ya kuheshimu haki za Uislamu kwa mwenye kusema: *"Laa ilaaha illa llahu Muhammad Rasulullahi."* Hivyo yeye ni Mwislamu na ana haki za Uislamu bila ya kutazama ni madhehebu yapi amefuata. Imekuja katika *Sahih al-Bukhariy*: "Mwenye kushuhudia kwamba hakuna Mungu isipokuwa Allah na akaelekea Kibla chetu, akaswali Swala yetu na akala chinjo letu basi huyo ni Mwislamu, anayo haki waliyonayo Waislamu na ni wajibu kwake yaliyo wajibu kwa Mwislamu."[4]

Na haya ndio yaliyopokewa katika tamko la mkutano wa Makka wa mwaka 1426 Hijiria, ambapo maazimio yalitilia mkazo suala la kutambua madhehebu za Kiislamu bila kujali tofauti zake, na kwamba wao wanakusanywa na anwani ya Uislamu, hivyo haijuzu kumwaga damu zao, kupora mali zao na kuvunja heshima zao.

Hapa tunarejea katika sira ya Imam Ali (as) ili tujue njia sahihi na ya sawa ya Kiislamu katika kutatua mas'ala ya tofauti za Kiislamu, hiyo ni kwa sababu tofauti baina ya makundi mawili makubwa kati ya Waislamu (nayo ni Shia na Suni) yalidhihiri baada ya kufariki Mtume (saww), wakati ambapo Shia waliona ni haki ya Imam Ali (as) kuwa Khalifa, na hiyo ni kwa sababu ya ubora wake kwao, na kwa wingi wa nususi zilizopokewa na pande zote mbili, ambapo wafuasi wa Ahlulbayt (as) wao wafahamu kutokana na nususi hizo haki ya uimamu wa Ali bin Abu Talib (as) baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), wakati ambapo Waislamu wengine wanaona kwamba ni kueleza tu ubora, nafasi yake na fadhila zake, hivyo ikhitilafu inapatikana katika kufasiri nususi, vinginevyo wanaafikiana katika

[4] Al- Bukhariy: Muhammad bin Ismail katika *Sahihil-Bukhariy*, Juz. 1, uk. 103 hadithi 939 Darul Kutubil ilimiyati Beirut

nususi nyingi, kama vile Hadith ya Ghadir, Hadith ya Thaqalain na hadith zingine ambazo sasa hivi hatuwezi kuzitaja na kuzielezea kwa ufafanuzi.

Imam Ali (as) aliishi katika hatua hiyo ngumu na hivyo ni wajibu wetu tufuate njia ya Imam Ali (as) katika kuamiliana kwake pamoja na wapinzani wake wakati huo. Amirul-Muuminina (as) alikuwa ni mtu wa umoja na ni kiongozi wake, wakati ambapo anaona yeye ndio mwenye haki katika ukhalifa na uimamu kama alivyosema hilo hapo baadaye katika moja ya hotuba zake iliyopokelewa kutoka kwake na maarufu kwa jina la Khutba ya Shaqishaqiyah, amesema (as):

أَمَا وَاللهِ لَقَدْ تَقَمَّصَها فُلانٌ، وَإِنَّهُ لَيَعْلَمُ أَنَّ مَحَلِّيَ مِنهَا مَحَلُّ
الْقُطْبِ مِنَ الرَّحَا، يَنْحَدِرُ عَنِّي السَّيْلُ، وَلا يَرْقَى إِلَيَّ الطَّيْرُ،

**"Naapa kwa Mwenyezi Mungu! Hakika fulani (Abu Bakr) ameuvaa (Ukhalifa) hali akiwa yuajua ya kwamba nafasi yangu kuhusiana nao (Ukhalifa) ni sawa na mahala pa muhimili wa jiwe la kusagia, maji ya mafuriko huniporomokea, wala ndege hawezi kunirukia ……."**[5]

Na alikuwa anaweza kujitokeza kutetea anayoyaitakidi kwamba ni haki yake, na alikuwa anajua kwamba kushika kwake ukhalifa ni maslahi kwa Ummah na ujumbe, lakini yeye aliona kwamba mapambano haya na msimamo huu utadhuru maslahi ya jumla katika wakati huo, na kwa hiyo hakutafuta haki yake hata alipojiwa na Abu Sufian na akawa anaita: "Hakika mimi naona ukelele hauzimwi ila kwa damu, enyi watu wa Abdu Manafi, kwa kitu gani Abu Bakr amechukua jambo lenu? Wako wapi wanyonge? Wako wapi wanyonge wawili, Ali na Abbas? Na kuna nini jambo linakaa kwa mtu

[5] *Nahjul- Balaghah*, khutuba ya 3

duni katika Makuraishi?" Kisha akamwambia Ali: "Nyoosha mkono wako nikupe kiapo cha utii. Wallahi kama unataka nitakujazia farasi na watu." Ali akamkemea na akasema: "Wallahi hakika wewe hukutaka isipokuwa fitina na hakika wewe Wallahi daima unautakia Uislamu shari, sina haja na nasaha yako."[6] Hakumkubalia na wala hakumkaribisha na hakutumbukia katika mtego ambao walikuwa wanautaka maadui wa Ummah, bali alitangaza:

**لَقَدْ عَلِمْتُمْ أَنِّي أَحَقُّ بِهَا مِنْ غَيْرِي، وَوَاللهِ لأُسْلِمَنَّ مَاسَلِمَتْ أُمُورُ الْمُسْلِمِينَ، وَلَمْ يَكُنْ فِيهَا جَوْرٌ إِلاَّ عَلَيَّ خَاصَّةً، الْتِمَاساً لِأَجْرِ ذلِكَ وَفَضْلِهِ، وَزُهْداً فِيمَا تَنافَسْتُمُوهُ مِنْ زُخْرُفِهِ وَ زِبْرِجِهِ**

**"Kwa kweli munajua kuwa mimi ni mwenye haki nao (ukhalifa) zaidi kuliko mwingine yoyote asiye kuwa mimi, na ninaapa kwa jina la Mwenyezi Mungu! Nitamwachia ukhalifa (Uthman) maadamu kumwachia yeye mambo ya Waislamu yatakuwa katika amani na dhulma haitokuwa isipokuwa kwangu tu, nikitaraji ujira wa hilo na fadhila zake, na kujiweka mbali na mnachoshindania na kujiweka kando na kuyafikia mapambo yake ambayo mnagombania."[7]**

Hakika Imam Ali alikataa kumpa kiapo cha utii Abu Bakr kwa siku kadhaa au miezi kadhaa kama zilivyotaja rejea za kihistoria, lakini alipoona ukubwa wa hatari ya kuritadi dhidi ya Uislamu, na uwezekano wa umoja wa Ummah kutetereka kwa kutokea ikhitilafu na mzozo wowote, aliingia chini ya bendera ya ukhalifa,

[6] Ibnul-Athir: 'Izzu diyn Abul- Hasan Ali bin Abi al- Karam katika *Al-Kaamil fiy Taarikh*, Juz. 2, uk. 10 chapa 1 mwaka 1408 Hijiria Muasasatu Tarikhil-Arabiy Beirut

[7] *Nahjul-Balaghah*, khutuba ya 73

kama anavyosema (as) katika maelezo yaliyopokelewa kutoka kwake:

**أَمّ َا بَعْدُ: فَإِنَّ اللهَ سُبْحَانَهُ بَعَثَ مُحَمَّداً صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَ سَلَّمَ نَذِيراً لِلْعَالَمِينَ، وَمُهَيْمِناً عَلَى الْمُرْسَلِينَ. فلمَّا مَضى _عَلَيْهِ السَّلَامُ_ تنَازَعَ الْمُسْلِمُونَ الْأَمْرَ مِنْ بَعْدِهِ. فَوَاللهِ مَا كَانَ يُلْقَى فِي رُوعِي، وَلاَ يَخْطُرُ بِبَالِي، أَنَّ الْعَرَبَ تُزْعِجُ هذَا الْأَمْرَ مِنْ بَعْدِهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَ سَلَّمَ عَنْ أَهْلِ بَيْتِهِ، وَلاَ أَنَّهُمْ مُنَحُّوهُ عَنِّي مِنْ بَعْدِهِ! فَمَا رَاعَنِي إلاَّ انْثِيَالُ النَّاسِ عَلَى فُلاَنٍ يُبَايِعُونَهُ، فَأَمْسَكْتُ يَدِي حَتَّى رَأيْتُ رَاجِعَةَ النَّاسِ قَدْ رَجَعَتْ عَنِ الْإِسْلاَمِ، يَدْعُونَ إِلَى مَحْقِ دِينِ مُحَمَّدٍ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَ سَلَّمَ فَخَشِيتُ إِنْ لَمْ أَنْصُرِ الْإِسْلاَمَ أَهْلَهُ أَنْ أَرَى فِيهِ ثَلْماً أَوْ هَدْماً، تَكُونُ الْمُصِيبَةُ بِهِ عَلَيَّ أَعْظَمَ مِنْ فَوْتِ وِلاَيَتِكُمُ الَّتِي إِنَّمَا هِيَ مَتَاعُ أَيَّامٍ قَلاَئِلَ، يَزُولُ مِنْهَا مَا كَانَ، كَمَا يَزُولُ السَّرَابُ، أَوْ كَمَا يَتَقَشَّعُ السَّحَابُ، فَنَهَضْتُ فِي تِلْكَ الْأَحْدَاثِ حَتَّى زَاحَ الْبَاطِلُ وَزَهَقَ، وَاطْمَأَنَّ الدِّينُ وَتَنَهْنَهَ.**

**"Ama baada ya hayo: Kwa hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu alimtuma Muhammad (saww) akiwa ni muonyaji kwa ulimwengu na shahidi wa Mitume. Mtume (saww) alipofariki, Waislamu walikhitilafiana kuhusu Ukhalifa baada yake. Naapa kwa Mwenyezi Mungu! Haikuingia akilini mwangu kwamba Waarabu watauhamisha Ukhalifa baada yake (saww) kutoka kwa Ahlulbayt wake (jamaa zake wa karibu), wala kwamba wao watauondosha kutoka kwangu. Sikufadhaishwa ila na kumiminika kwa watu kwa fulani, wakimpa kiapo cha utiifu. Niliuzuwia mkono wangu mpaka pale nilipoona kurejea kwa watu (kwenye ukafiri) wakiwa mbali na Uislamu, wakiwa wanalingania katika kuifuta Dini ya Muhammad (saww). Basi niliogopa ikiwa sitounusuru Uislamu na watu wake, kwa kuona dosari humo au mmong'onyoko, juu yangu itakuwa msiba mkubwa zaidi kuliko kuukosa Ukhalifa wenu ambao ni starehe ya siku chache, hutoweka kilicho kuwa kama yatowekavyo magazigazi, au kama yanavyotawanyika mawingu. Nikasimama katika matukio yale mpaka batili ilitoweka na kuyeyuka, na Dini kubaki katika amani na salama."[8]**

Hakika Ali bin Abu Talib alibeba jukumu lake. Alikuwa pamoja na Makhalifa na pamoja na Ummah, anahudhuria msikitini na anashiriki katika Swala ya jamaa, anashauriwa na anashauri na kutoa rai yake na anaunusuru Ummah. Na aliwasaidia Makhalifa katika misimamo mingi. Kuna zaidi ya sehemu tisini katika mambo ya kijeshi, kiuchumi, kisiasa na kidini, ambamo Khalifa Umar alimshauri Imam Ali (as) na akachukua rai yake, ameziandika pamoja na kutaja rejea zake Sheikh Najmi Diyn al-Askariy katika kitabu chake *Aliyu Wal- Khulafaai*.[9]

Na kwa hiyo tunauliza: Vipi alikuwa anataka ushauri kwa Ali bin Abu Talib kama alikuwa hamwamini Ali (as) na hana imani na rai yake? Ali (as) hakuwa anawatazama Makhalifa kama maadui wala kuficha uadui na kwenda mbio kulipiza kisasi kwao, na wao walikuwa wanamwangalia Ali (as) kama mshauri katika yale ambayo

[8] *Nahjul-Balaghah*, Barua ya 62.
[9] Al-Askariy: Najmi Diyn katika *Aliyu Wal-Khulafaai*, Chapa ya al-Adab Najaf 1380 Hijiria.

yana maslahi ya Ummah na dini, vinginevyo kama Umar na Abu Bakr wangekuwa wanamwangalia Ali (as) kama adui basi wasingerejea kwake na kuamini rai zake, na Imam Ali - mukabala wa hilo – asingeamiliana nao vizuri kutokana na uadui binafsi, bali alikuwa anawapa nasaha na anawashauri katika yale ambayo yana maslahi ya Ummah na Waislamu kwa wakati huo, hadi imepokewa kutoka kwa Khalifa Umar kwamba alikuwa anajikinga kwa Mwenyezi Mungu asitokewe na tatizo wakati ambapo Ali hatokuwepo.[10] Imepokewa kutoka kwa Yahya bin Aqil – kama ilivyo katika *Dhakhairul-Uqbaa* – kwamba Umar alimwambia Ali (as) na alikuwa ameshamuuliza jambo akamjibu: "Najikinga kwa Mwenyezi Mungu kuishi katika siku ambayo hatokuwepo humo Abu Hasan." Na imepokewa – pia – "Kama sio Ali angeangamia Umar."[11] Na dua yake vilevile: "Eee Mwenyezi Mungu! Usiniteremshie shida isipokuwa na Abu Hasan awepo karibu yangu."[12] Na nususi ziko nyingi katika vitabu vya historia na vitabu vya pande mbili.

Pamoja na kwamba Imam Ali (as) alionyesha kutoridhika kwake na baadhi ya siasa za wakati wa Uthman na hususan nafasi ya wapambe ambao walikuwa karibu na Khalifa, isipokuwa hakuacha kumpa Uthman nasaha na rai, na alijaribu sana kutatua maudhui ya uasi dhidi ya Khalifa. Alikuwa ni mtu wa katikati na balozi baina ya wapinzani na Khalifa zaidi ya mara moja, lakini jambo lilitoka mikononi mwake na alipozingirwa Uthman na akazuiwa maji alitaka msaada kwa Ali. Imam akawatuma watoto wake Hasan na Husain na kiriba cha maji ili wakiingize kwenye nyumba ya Uthman.[13]

---

[10] Al-Mutaqiy al-Hindiy katika *Kanzul-Umaal*, Juz. 10, uk. 300 Hadith 29509.

[11] Rejea iliyotangulia uk. 149.

[12] Rejea iliyotangulia uk. 149.

[13] Twabariy: Muhammad bin Jarir katika *Tarikhul-Umami wal-Muluuk*, Jz. 3, uk. 417 muasastual- ilamiy lilimatubuaati Beirut

Na katika nususi za kihistoria imetajwa katika vitabu vya Sunni na Shia kwamba aliamuru watoto wake Hasan na Husain (as) wabakie katika mlango wa Uthman kwa ajili ya kumlinda,[14] lakini wapinzani walipenya katika nyumba za jirani na kuingia katika nyumba ya Khalifa.

Hivi ndivyo alivyokuwa Ali bin Abu Talib (as), na hivi ndivyo inapasa uwe mfumo wa wapenzi wake na wafuasi wake. Hadi mwisho wa pumzi ya uhai wake (as) alikuwa anajali Ummah, alikuwa anajua kwamba muuwaji wake muovu Ibnu Muljim anahusiana na Khawariji, na alikuwa anajua kwamba wao wamemsukuma kufanya kosa hili, lakini hakutaka kuuliwa kwake iwe ni sababu mpya ya tatizo katika hali ya Ummah, na hivyo alisema katika wasia wake:

**يَا بَنِي عَبْدِالْمُطَّلِبِ، لاَ أُلْفِيَنَّكُمْ تَخُوضُونَ دِمَاءَ الْمُسْلِمِينَ خَوْضاً، تَقُولُونَ: قُتِلَ أَمِيرُالْمُؤْمِنِينَ. أَلاَ لاَ تَقْتُلُنَّ بِي إِلاَّ قَاتِلِي.انْظُرُوا إِذَا أَنَا مِتُّ مِنْ ضَرْبَتِهِ هذِهِ، فَاضْرِبُوهُ ضَرْبَةً بِضَرْبَةٍ، وَلاَ يُمَثَّلُوا بِالرَّجُلِ، فَإِنِّي سَمِعْتُ رَسُولَ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَمَ يَقُولُ: إِيَّاكُمْ وَالْمُثْلَةَ وَلَوْ بَالْكَلْبِ الْعَقُورِ.**

**"Enyi wana wa Abdul Muttalib! Sitaki niwakute mnaingia katika damu za Waislamu kwa kusema: 'Ameuliwa Kiongozi wa Waumini.' Tambueni kwamba, msimuue kwa ajili yangu yeyote isipokuwa yule tu aliyeniua. Angalieni, iwapo nitakufa kwa sababu ya pigo lake hili, basi mpigeni pigo moja kwa pigo moja, wala msimfedheheshe mtu**

[14] Ibnu Qutaibah: Abdillahi bin Muslim katika *al-Imamatu wa Siyaasa*. Juz. 1, uk. 42 muasastul-halabiy washurakaahu

**(maiti kwa kumkata kata viungo vyake), kwani mimi nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) akisema: 'Tahadharini juu kumfedhehesha maiti hata kama ni mbwa mkali."[15]**

Hakika sira ya Ali inatilia mkazo ikhilasi yake ya kina katika dini na kujali kwake sana juu ya umoja wa Ummah, kwani yeye anamwabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuhifadhi umoja na anashikamana nao kama njia ya kupata thawabu za Mwenyezi Mungu na radhi yake. Umoja ni msingi wa dini na ni wajibu wa kisharia kabla ya kuwa ni jambo la kisiasa au maslahi ya wakati, amesema kweli Amirul-Muuminina (as) aliposema:

**وَلَيْسَ رَجُلٌ ـ فَاعْلَمْ ـ أَحْرَصَ عَلَى جَمَاعَةِ أُمَّةِ مُحَمَّدٍ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ و أُلْفَتِهَا مِنِّي، أَبْتَغِي بِذلِكَ حُسْنَ الثَّوَابِ، وَكَرَمَ الْمَآبِ، وَسَأَفِي بِالَّذِي وَأيْتُ عَلَى نَفْسِي، وَإِنْ تَغَيَّرْتَ عَنْ صَالِحِ مَا فَارَقْتَنِي عَلَيْهِ.**

**"Na (jua kuwa) hapana mtu mwenye hima ya umoja wa Ummah wa Muhammad (s.a.w.w.) na usuhuba wao kuliko mimi, kwa kufanya hilo ninataka malipo mema, na marejeo ya heshima. Nitatekeleza niliyoahidi katika nafsi yangu, japo yabadilike mema ambayo uliniacha nayo."[16]**

---

[15] *Nahjul-Balaghah*, khutba ya 47
[16] *Nahjul- Balaghah*, barua ya 78

# UPANDE WOWOTE HAUNA HAKI YA KULAZIMISHA RAI YAKE KATIKA JAMII[17]

Sheikh Hasan Safar amesema kwamba ukandamizaji katika rai za watu umeshamalizika na si haki kwa upande wowote kuikandamiza jamii katika maelekezo yake tu, na ni lazima tuwe na subira ili kuweza kuvumilia hali ya rai nyingi. Maelezo hayo yamekuja katika muhadhara alioutoa jioni ya siku ya Jumatano katika uwanja wa Shawikah huko Qatif katika kumbukumbu ya siku ya kufa shahidi Imam Ali (as). Safar aliongeza kwa kusema kwamba kizazi cha leo kinalazimika kumsoma kwa juhudi Imam Ali (as) kulingana na mazingira ya leo bila kuishia tu kusoma vizazi vilivyopita. Pia ameongeza kwa kusema kama kuna aliyetosheka ndani ya nafsi yake kumsoma Ali (as) katika upande wa miujiza ya shakhisiya hiyo au katika upande wa huzuni tu, basi ajue hakika kusoma kwa namna hiyo kumekuja kama matokeo ya kizazi kilichoshindwa, kilichojifungia katika dhati yake, nacho hakinasibihiani kabisa pamoja mfumo wa fikra ya Ali na mtazamo wake.

Muhadhara ambao umekuja kwa anwani ya "Umoja" haukuepukana na madhumuni yanayozungumzia umoja wa Kiislamu, ambao Sheikh Safar anaona kwamba haumaanishi kamwe kufuta sifa makhususi za siasa au za madhehebu za upande wowote. Na ameongeza kwamba umoja unamaanisha kujikita katika sehemu za ushirikiano na maslahi ya jumla ya Ummah, katika mazingira ambayo humo wote hupewa ruhusa na fursa ya kutoa rai zao bila ya upande mmoja kuukandamiza upande mwingine wowote ule. Na Sheikh Sa-

[17] Imesambazwa katika tovuti *raswidal-khabar* tarehe 12/10/2006

far ameona kwamba kuna mielekeo mitatu katika umoja; wa kwanza ni Umoja wa Kijamii, wa pili ni Umoja wa Kitaifa, na wa tatu ni Umoja wa Ummah.

Na akaongeza kwamba Umoja wa Kijamii haumaanishi kwa hali yoyote ile kuwaunganisha wote katika mfumo mmoja na fikra moja na kundi moja, hiyo ni kinyume na tabia ya kibinadamu, na zimekwisha zama za ukandamizaji katika rai za watu katika jamii yetu. Na ameashiria kwamba ni muhimu katika upande huu kusimamisha uchochezi, na kueneza hali ya usamehevu badala yake, sambamba na kujongea kwenye taasisi za kijamii na kufanya uwezo kuwa ndio msingi, na sio dhana na utashi binafsi.

Ama katika upande wa Umoja wa Kitaifa ameona kwamba Ummah unalengwa na nguvu za nje, hivyo ni lazima kuziba mianya ya ndani kwa kutoa haki kwa wote na kusimamisha hali za uchochezi na kumaliza fitina. Na ameongeza kwamba haijuzu kuzuia watu kutumia uhuru wao wa kidini kwa madai ya kupiga vita makundi, na wala uhuru wa kutoa mawazo haujawahi hata siku moja kuwa dhidi ya Umoja wa Kitaifa.

Ama katika upande wa Ummah, Sheikh Safar ameona kwamba kila mwenye kushuhudia shahada mbili basi inahifadhiwa damu, heshima na mali kama ilivyo katika athari, na hayo yameelezwa katika maafikiano ya mkutano wa Makka ambao ulitambua madhehebu nane ya Kiislamu. Sheikh Safar ametaka katika maudhui haya kumfuata Imam Ali (as), katika wakati ambao hakuacha haki yake hata siku moja ila alijitahidi sana kuulinda Ummah kutokana na mfarakano. Ameongeza kwamba Ali (as) hakuwa mwenye kukaa ndani ya nyumba yake kama wanavyoona baadhi bali alifanya kazi pamoja na Makhalifa katika kuwapa ushauri na nasaha hadi neno "Najikinga kwa Mwenyezi Mungu kuishi katika siku ambayo hatokuwepo humo Abu Hasan." likawa mashuhuri.

Ametaja kwamba muhadhara umekuja kufuatia ratiba ya "Ali na Ummah" ambayo iliandaliwa na kitengo cha Imam Hasan katika uwanja wa Shawikah na iliendelea kwa muda wa siku mbili.

# IMAM ALI (AS) NI KIONGOZI WA UREKEBISHAJI

Kumekuwa na aina nyingi za kusoma shakhisiya ambazo zimechukua nafasi katika fikira ya vizazi vya leo na vijavyo katika maisha yao, kwa kurithi kutoka kwao mitazamo na misingi au kuyafikisha matamko ya nadharia hizo katika sekta ya utekelezaji wa kivitendo. Na kwa sababu tupo katika kumbukumbu ya mmoja kati ya watukufu wa ubinadamu na kiongozi wake katika fikra na mwenendo, naye ndio kiongozi wa urekebishaji, Amirul-Muuminina Ali bin Abu Talib (as), kiongozi ambaye amesomwa na wengi kati ya wanafikra na maarifa, na hatimaye baadhi wakavuka mpaka na wengine wakamteremsha hadhi, kama alivyotabiri yeye mwenyewe aliposema: “Wameangamia kwa ajili yangu watu wawili: Mwenye kunipenda kupita kiasi na mwenye kunichukia na kuniteremsha.”[18]

Na ili tusiwe moja ya aina mbili, tunajaribu kumsoma Imam Ali (as) kwa usomaji utakaonyoosha yale ambayo yamepindishwa miongoni mwa tabia katika hali yetu ya leo. Tunaachana na usomaji wa kuiga ambao unatushughulisha na huzuni ya historia iliyopita, matatizo yake na matukio yake, sisi tuna haja ya kusoma historia ya Kiislamu na historia ya viongozi wake kwa usomaji mpya utakaotusaidia katika kutatua mambo yetu na kunyanyua kiwango chetu na kuondoa hali yetu mbaya. Hatuna haja na usomaji utakaoongeza hali ya chuki na bughudha baina yetu, na kuzama katika matatizo yaliyopita na matukio yake, isipokuwa kwa kiwango kitakachotupa somo na mazingatio, na kwa hiyo tunazungumzia juu ya sira ya Imam Ali (as) katika urekebishaji.

[18] Sharifu Ridhaa: katika *Nahjul-Balaghah* hekima namba 113 kimehakikiwa na Muasasatu Nahjul-Balaghah chapa ya 3 mwaka 1416 Hijiria.

## 1. Falsafa ya Kurekebisha:

Jamii ya binadamu daima inahitaji uchunguzi wa kudumu na utafiti wenye kuendelea kuhusu hali yake na mazingira yake. Hiyo ni kwa ajili ya kutatua nukta za kasoro na mapungufu, kwa sababu kila jamii ya binadamu haiepukani na nukta za udhaifu unaohitaji kupewa nguvu, au mianya inayohitaji kuzibwa ili jamii hiyo ifike katika safu ya jamii zilizoendelea. Hakika kasoro ambazo jamii ya binadamu yoyote haisalimiki nazo zina sababu nyingi, hapa tutaeleza tatu miongoni mwazo:

## 2. Kuwepo kosa:

Hakuna yeyote anayeweza kudai umaasum na ukamilifu isipokuwa maasumina ambao Mwenyezi Mungu amewahifadhi. Ama jamii, viongozi na makundi, kwao kuna uwezekano wa kutokea makosa: "Kila binadamu anakosea na aliye mbora kati ya wanaokosea ni yule mwenye kutubia." Kama ilivyopokewa kutoka kwake (saww).[19]

Ummah unaweza kuchukua mwelekeo wa kimakosa, na uongozi unaweza kufuata mfumo usio sahihi, na mwanachuoni au kundi la maulamaa linaweza kutoa rai na fikra zilizo mbali na ukweli, na hili ni jambo lipo, hakuna yeyote anayeweza kukataa, na maadamu kosa hili lipo katika maisha ya jamii basi ni juu ya jamii katika kila hatua na kila wakati kutafiti kisha kuuliza: Je, hili si kosa katika mwelekeo wetu? Je, hili si kosa katika rai zetu?

## 3. Kuwepo upotuvu:

Hakuna ubishi kwamba watu katika jamii ya kibinadamu sio malaika na sio maasumina ambao haitokei kwao upotovu. Unaweza kupati-

[19] Al- Hakim Anisaburiy katika *al- Mustadrakus-Sahihain*, Juz. 4 hadithi ya 17/7617 Darul-Kutubil- ilimiyati chapa 1 mwaka 1411Hijiria Beirut

kana upotovu katika kundi la mbele katika Ummah au kwa watu wa kawaida, au kutoka katika nguvu za katikati zinazounganisha baina ya viongozi wa Ummah na watu wake.

Upotovu huu unaweza kuwa wa kudhamiriwa au wa kutokudhamiriwa, unaweza kutokea katika utoaji rai au katika utekelezaji wa mpango na mikakati. Hivyo ni juu ya jamii kuhakikisha usahihi wa mwenendo wake na kutopatwa na upotovu, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَمَا أُبَرِّئُ نَفْسِي إِنَّ النَّفْسَ لَأَمَّارَةٌ بِالسُّوءِ إِلَّا مَا رَحِمَ رَبِّي
إِنَّ رَبِّي غَفُورٌ رَحِيمٌ

**“Nami sijitakasi nafsi yangu; hakika nafsi ndiyo iamrishayo mno uovu, isipokuwa ile ambayo Mola Wangu ameirehemu. Hakika Mola Wangu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.”**

**(Surat Yusuf: 53)**.

## 4. Tabia ya ustawi na kuendelea:

Rai inaweza kuwa sahihi, na mwelekeo sahihi kwa muda maalum, na mazingira maalum, lakini hali inapobadilika na maisha kuboreka hakika maamuzi hayo yanahitaji mabadiliko na kuboreshwa. Hivyo kama hakuna ufuatiliaji katika mabadiliko na kuboresha mambo lazima kutatokea kasoro, na kasoro hii sio matokeo ya rai yenyewe na sio kwa kuwepo upotovu, hakika ni matokeo ya kutokufuatilia mabadiliko. Na kwa hivyo hakika jamii zilizoendelea na kustaarabika zinajua haja ya kuchunguza, kutafiti na kuhakiki mabadiliko ili kubadilisha na kurekebisha, ambapo kwa mtazamo wa haraka

katika kila katiba ya nchi hizo, tunakuta katika katiba kuna ibara inayozungumzia uwezekeno wa kuboresha na kufanya mabadiliko katika ibara za katiba, pamoja na kwamba katiba inahesabiwa ni kitu cha thamani zaidi katika kila Ummah, kwa sababu katiba inawekwa baada ya kudurusu, kutafiti na kura ya maoni ya wananchi, na inaambatana na hatua na dhamana mbalimbali, lakini kwa sababu hali inabadilika na kwa sababu kosa linaweza kutokea, inapatikana katika kila katiba kati ya nchi kifungu kinachotatua namna ya kubadilisha na kuboresha katiba. Je, wabunge kwa uwingi wake wanapiga kura ya mabadiliko? Au haja ndio inahitajia kura ya maoni ya wananchi katika kila mabadiliko?

Hakika kuwepo kifungu kinachotatua maudhui ya mabadiliko katika katiba ni dalili inayotutaka tujue umuhimu wa mabadiliko na maboresho hata katika katiba, nayo ndio nyaraka thabiti zaidi na kitu cha thamani zaidi katika kila Ummah.

Katika upande mwingine utakuta jamii zilizoendelea zina taasisi zinazoshughulika na kufuatilia mabadiliko na maboresho. Bunge lake na taasisi zake za kikatiba, kisiasa na kielimu, zote zinalengwa katika kufuatiliwa na kukaguliwa ili kufanyiwa mabadiliko na maboresho kadiri ya mahitajio. Na kuna vituo mbalimbali vya utafiti na masomo vinavyochunguza na kusoma hali mbalimbali za kijamii, kiutamaduni na za kisiasa, na kupendekeza mabadiliko au utatuzi, na kuonesha nukta za udhaifu uliopo. Na pia kuna uangalizi wa rai ya jamii ya kuainisha na kutoa maoni. Na katika kila tukio au jambo huwa kuna uangalizi wa rai ya jamii katika utekelezaji wa idara ya kisiasa na katika hali ya kijamii = Hizi ni nguvu tatu zilizopo katika jamii zilizoendelea: Taasisi rasmi, vituo vya utafiti na uchunguzi, maoni ya jamii. Nguvu hizi ni mifumo inayoshughulikia mapitio kwa ajili ya mabadiliko na urekebishaji.

**Ugumu wa kufanya mapitio na kuboresha:**

Katika jamii zetu za Kiarabu, (Kiafrika) na za Kiislamu mambo haya ni nadra kufanyika na ni duni, na katika baadhi ya sekta hakuna kabisa mapitio, na kwa ajili hiyo jamii zetu haziishi katika hali ya kufanya mapitio, kutafiti na urekebishaji wa daima.

Jamii nyingine zinatekeleza urekebishaji na uboreshaji wakati zinapofanya marejeo katika hali zake, wakati ambapo mara nyingi katika jamii zetu kufanya marejeo inakuwa ni jambo gumu, kubadilisha na kuboresha inashindikana, na kwa sababu hiyo hali inabaki kama ilivyo katika makosa na upotovu, ikiwa ni pamoja na kurudi nyuma katika msafara wa maendeleo ya maisha na jamii. Unabaki katika hali mwendelezo na kufuata kana kwamba tunafanana na yaliyonukuliwa kutoka kwa juha alipoulizwa wakati mmoja:

Una miaka mingapi?

Akasema: Nina miaka arobaini. Na baada ya miaka ishirini akaulizwa: Una miaka mingapi? Akasema: Miaka arobaini. Alipoulizwa kwa nini: Akasema: Neno la mtu mmoja halibadiliki.

Maadamu tunapita katika rai makhususi na hali maalum basi inapasa tuendelee nayo

إِنَّا وَجَدْنَا آبَاءَنَا عَلَى أُمَّةٍ وَإِنَّا عَلَى آثَارِهِمْ مُقْتَدُونَ

**"Hakika sisi tuliwakuta baba zetu juu ya desturi na tunafuata nyayo zao."** **(Surat Zukhruf: 23).**

Katika jamii nyingi za Kiarabu, (Kiafrika) na za Kiislamu, kufanya marejeo ni jambo gumu, katika nyanja za kisiasa na kifikra, katika ada na mila, bali hata katika baadhi ya zana na vyombo vya nje tunakuta kufanya mabadiliko ni jambo gumu.

Nimesoma katika jarida la *Al-Madinah* katika kiambatanisho cha risala ya tarehe 30 Shawwal 1426 Hijiria, mazungumzo ya Spika wa Bunge la Saudia, Sheikh Swalehe bin Hamid naye ni Imam wa Msikiti Mtukufu wa Makka, alikuwa akizungumza katika hafla ya karamu iliyofanyika katika Chuo Kikuu cha Ummul-Quraa, kwa ajili ya mzazi wake Sheikh Abdillahi bin Muhammad bin Hamid (1329 – 1402 Hijiria). Katika mazungumzo yake alizungumzia namna gani mzazi wake aliweza katika miaka ya sabini kushinda vita vya kujenga ukumbi mkubwa kwa simenti huko Baridah, baada ya kupata upinzani mkali kutoka kwa watu wa Madina ambao walipinga kwa nguvu zote kutumia simenti katika ujenzi huo na wakamtaka jengo liwe kwa udongo na makuti ya mitende, kama walivyokuwa baba zao, huku wakizingatia kwamba hiyo ni vita ya uhai au mauti.

Huu ni mfano wa kukataa mabadiliko na maboresho hata katika njia na vifaa, mfano wa hayo tunaukuta katika jamii zetu mbalimbali. Sheikh Dr. Ahmad al- Waailiy (aliyezaliwa mwaka 1347 na kufariki mwaka 1424 Hijiria) katika kitabu chake *Tajaarubiy Ma`al-Mimbar* anazungumzia mradi aliouanzisha yeye na baadhi ya maulamaa wenye kuelewa huko Najaf Tukufu, kwa ajili ya kusaidia kuendeleza na kukuza kiwango cha hotuba na makhatibu. Hivyo walikodi sehemu kama kituo kwa jina la Klabu ya Usambazaji. Anasema: “Watu wenye maslahi binafsi wakaanzisha upinzani na miongoni mwao ni kundi la wanaojifunza namna ya kutoa hotuba, hivyo habari zikaenea zikisema: “Hakika Klabu ya Usambazaji inataka kubadilisha sura ya Bani Ummaiya katika macho ya watu na kutokomeza maadhimisho na mafunzo ya Husain na kupotosha historia.” Hadi mwisho wa ma-

dai yao ambayo yalikuwa na uongo uliopelekea kupatikana tamko kutoka kwa wakuu wa kidini linaloilaumu Klabu ya Usambazaji. Na mambo yakamalizikia kwa kushambuliwa taasisi iliyoandaliwa kufundisha na klabu ya usamabazaji pia, viti vikavunjwa na jengo na miundombinu ikabomolewa, na wasimamizi wakakimbia na kujificha mbali na watu. Na moja ya tamko kutoka kwa baadhi ya viongozi wa kidini lilikuwa ni kwamba Husain (as) ameuliwa mara mbili, Siku ya Ashura na Siku ya Harakati za Klabu ya Usambazaji."[20]

Inanidhihirikia kwamba kuna sababu mbili zinazofanya kuwepo na ugumu wa kufanya marejeo, mabadiliko na maboresho katika jamii zetu:

**Kwanza:** Utamaduni unaozuia mabadiliko, ambao unasimama kwa msingi wa kutukuza hali iliyopo na kuikweza, ambapo huonekana hakuna uwezekano wa kuleta zuri zaidi ya lililopo. Kisha kuuchanganya utamaduni huu na nadharia ya njama kutoka kwa maadui, kwani matatizo ya Ummah ni njama za Mayahudi, Manaswara na mbinu za ubeberu wa kilimwengu. Hakika hakuna yeyote anayekataa kwamba nguvu za kigeni zina tamaa zake na maslahi yake na kwamba zinaenda mbio kututawala kwa kiwango cha ulimwengu, lakini udhaifu wetu ndio ambao unawapa tamaa na mwanya ambao unawawezesha wao kufaulu katika mbinu zao na mikakati yao dhidi yetu.

Sisi tuna haja ya urekebishaji wa kidini. Utamaduni wetu wa kidini unahitaji marekebisho. Dini ni ya haki, lakini tunachokifahamu katika dini kinahitaji kurejewa, wengi wanachanganya baina ya dini na uhalisia wake na baina ya ufahamu wa watu katika dini, maulamaa hawadai kwamba wanapatia katika rai zao kwa uhakika wa mia kwa mia, bali wanasema hakika wao wanajitahidi na mwenye ku-

[20] Al-Waailiy Dr. Ahmad katika *Tajiribatiy ma'al- mimbar* uk. 185 Daru Zahraa chapa 1 mwaka 1998 Beirut

jitahidi anaweza kupatia na kukosea, na maana ya hilo ni kwamba mlango wa ijtihadi ni wajibu uwe wazi. Kwa nini inakuwa vigumu kwetu kuboresha na kurekebisha katika rai na fikra nyingi, hadi hata vipengele vya mas'ala tunavihesabu ni katika dharura na thabiti za kiitikadi na dini, na kati ya vitu vigumu ambavyo haiwezekani kuangaliwa upya?

Umezindua mtazamo wangu utafiti aliouandika mmoja wa mafaqihi wakubwa wa huko Najaf Tukufu, Sheikh Muhammad Is'haq al-Fayadh chini ya anwani ya Hukumu za Ijtihadi, humo anaashiria kwamba fungu la hukumu za kisharia ambazo zina hali thabiti isiyotegemea juhudi za faqihi, kazi ya ijtihadi na uchambuzi, na ambazo hazina hitilafu baina ya mafaqihi na mujtahidina, ni asilimia sita tu kati ya asilimia mia moja ya hukumu zote za kisharia. Hivyo asilimia tisini na nne iliyobakia ni hukumu za kisharia ambazo zina hali ya kinadharia inayotegemea kazi ya ijtihadi na uchambuzi, na inakuwa ni sehemu ya utafiti na ikhitilafu baina ya mafaqihi na mujtahidina.[21]

Hivyo sisi tuna haja ya urekebishaji wa jumla katika nyanja mbalimbali. Lakini kikwazo ni kuwepo utamaduni huu ambao unatukuza uhalisia na wala hautoi fursa kwa rai yoyote, wala kwa ukosoaji wowote katika nyanja ya kidini, na kana kwamba ukosoaji wowote ni kukosoa dini. Katika mambo yasiyo na shaka ni kwamba ukosoaji wenye udhibiti wa kielimu na wa kimaudhui sio kukosoa dini. Dini ina nguvu na ni ya kina, haiogopewi, na ukosoaji unaipa dini nguvu, na kufanya marejeo kunadhihirisha kina cha dini, na kunadhihirisha mamlaka yake. Kisha ni anayekabiliwa na udhaifu katika rai yake na katika hoja zake ndiye anayeogopa kudhihirisha udhaifu wake, na sio dini, kwani ukosoaji unafikisha kwenye hali bora zaidi katika sekta za kidini na katika nyanja za kisiasa pia. Hivyo ni wajibu ku-

[21] Al-Fayadh: Sheikh Muhammad Is'haq katika Masaailul-Mustahadatha uk: 7 Muasasatu ma'arifiy – Kuwait 2005

wepo na ukosoaji unaolenga kupanua wigo wa ushirikiano wa wananchi, na kuweka dhamana itakayowawezesha kuchukua maamuzi magumu na sahihi, ili kuweka zana za utendaji na utekelezaji mbali na ufisadi na dhana, na hivyo kuwepo uangalizi wa serikali, uhuru wa kisiasa na wa vyombo vya habari unaowezesha kufichua mchezo wowote mchafu au ufisadi. Na hali ni hiyo hiyo katika nyanja ya kijamii, ni lazima kutoa fursa ya ukosoaji na kuwepo taasisi mbalimbali za wananchi zenye harakati.

**Pili:** Kuwepo kwa vituo vyenye nguvu vinavyonufaika kutokana na hali iliyopo, na vinavyoogopa mabadiliko na mageuzi kwa ajli ya maslahi yake na mapato yake, na kwa hiyo vinapinga kufanya marejeo, mabadiliko, maboresho na marekebisho, ili mambo yabaki kama yalivyo kwa sababu vituo hivyo vinafaidika kwa kulinda maslahi yake na mapato yake.

## SABABU ZA UREKEBISHAJI NA MAGEUZI:

Kwa ajili ya kupata mwamko wa urekebishaji na mageuzi katika nyanja yoyote ile ya maisha ya Ummah ni lazima kupatikane sababu tatu:

**Kwanza:** Kujitolea kwa Viongozi:

Uongozi wa kidini na kisiasa katika Ummah ni wajibu ujitolee na kupambana kwa ajili ya urekebishaji na mageuzi, vinginevyo hali itatahadharisha juu ya hatari kubwa. Ulimwengu hautoturuhusu sisi kubaki katika hali tuliyomo, madhara ya hali ya kutoendelea ambayo tunaishi nayo sio tu inatukabili sisi tu, bali ulimwengu umekuwa unakabiliwa na cheche zake na matokeo yake. Ulimwengu haukubali Ummah huu ubakie kuwa ni kikwazo mbele ya harakati za uboreshaji wa kiulimwengu. Kama ambavyo pia kuna tamaa na malengo

ya maadui na mielekeo dhidi ya Ummah na maslahi yake, hivyo maadui huitumia fursa hii ya kutoendelea ili kusheheneshа mashambulizi yake katika Ummah kwa lengo la kutawala matakwa yake na utajiri wake. Na kuna kuchoshwa na ghadhabu ndani ya jamii za Ummah, hivyo ikiwa hakutakuwa na juhudi zozote za kuanza urekebishaji na mabadiliko ya kubadili hali hii basi kutatokea mlipuko na majanga.

Na mielekeo hii ya kigaidi ya kimabavu si kingine isipokuwa ni cheche za matatizo na hali mbaya ambayo Ummah unaishi nayo, na matokeo ya baadaye ni hatari zaidi ikiwa hakutakuwa na juhudi za kujitolea kutoka kwa viongozi wa Ummah kwa ajili ya kurekebisha na kuboresha. Na hapa tunathamini na kupongeza kujitolea kulikofanywa na kiongozi wa Haram mbili tukufu Mfalme Abdillahi bin Abdul-Aziz, alipowaita viongozi wa Ummah na maulamaa wake katika mkutano wa Makka Tukufu kabla ya miaka miwili iliyopita, ili kuweka mkakati wa kuleta mabadiliko yenye uboreshaji. Kisha ukafanyika mkutano wa viongozi wa nchi za Kiislamu mwezi 5 na 6 Dhul-Qaad 1426 Hijiria, kwa ajili ya kujadili maelekezo ambayo yalitolewa na Maulamaa na wanafikira, na hatimaye yakapita, yakakubaliwa na kuafikiwa, lakini vipi kuhusu utekelezaji wa kivitendo wa maamuzi hayo kwa upande wa dola na vyama vya kisiasa?

Ni wajibu haya yatekelezwe kivitendo na kila dola na kila jamii, na sio tu kupendekeza nadharia, kwani Ummah uko njiapanda na unakabiliwa na hatari na janga kubwa. Tunahitaji kujitolea kwa ujasiri na ushujaa, kwa sababu uongozi wowote wa kisiasa unaotaka urekebishaji hautopata njia iliyotandikwa maua na manukato mbele yake, bali kuna vikwazo na vituo vya nguvu za ukandamizaji, hivyo uongozi wowote wa kidini unaotaka kurekebisha na kuleta mabadiliko ya kimaendeleo hautopokelewa kwa maamukizi, salamu, shangwe na heshima, bali kutakuwa na uchochezi dhidi ya uongozi huo

na utatuhumiwa katika dini yake, lakini mambo yanahitajia kujitolea na ikhilasi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kama anavyosema Yeye Mwenyewe (swt):

الَّذِينَ يُبَلِّغُونَ رِسَالَاتِ اللَّهِ وَيَخْشَوْنَهُ وَلَا يَخْشَوْنَ أَحَدًا إِلَّا اللَّهَ وَكَفَى بِاللَّهِ حَسِيبًا

**"Ambao walifikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu na kumwogopa Yeye, wala hawamwogopi yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu Ndiye anayetosha kuhesabu." (Surat Ahzab: 39).**

**Pili:** Utamaduni wa Kurekebisha:

Uongozi wowote unaotaka kufanya marekebisho na kuleta mabadiliko unapasa kutafakari katika kuzalisha utamaduni wenye kusaidia kuleta maelekezo ya urekebishaji, kwa sababu haiwezekani kutokea urekebishaji katika mazingira ya utamaduni usioendelea. Ni lazima kushajiisha utamaduni wa uwazi na uelewa wa kujua mahitaji ya wakati, na kutoa fursa ya uhuru wa kutoa rai na maoni katika upeo wa kisiasa, kidini na kijamii.

**Tatu:** Harakati za Watu:

Uelewa wa watu wa Ummah na mwitikio wao katika mpango wa urekebishaji na mageuzi, ndio unaoruhusu kuanza mwamko wa urekebishaji. Ama kuishia tu kutoa kauli na matamanio ya mageuzi bila ya kunyanyua kiwango cha harakati na uzalishaji, na kujongea karibu na uongozi wenye ikhilasi na mpango unaofaa, hakika jambo hilo halitobadilisha chochote katika hali ya Ummah.

# IMAM ALI ANAPAMBANA KWA AJILI YA KUREKEBISHA MAMBO:

Na tusogelee sira ya Amirul-Muuminina Ali bin Abu Talib (as) ambapo tunaweza kusema kwa haki kabisa kwamba hakika ni kiongozi wa urekebishaji katika zama za mwanzo za historia ya Ummah wa Kiislamu, ambapo alifuata mfumo jasiri wa urekebishaji. Alifika katika ukhalifa kwa kupewa kiapo cha utii  na wananchi, ambapo ni tofauti na kiapo cha utii walichopewa makhalifa waliomtangulia. Ambapo Khalifa Abu Bakr alifika kwenye ukhalifa kwa njia ya kupewa kiapo cha utii katika ukumbi wa Saqifa Bani Saad, na Khalifa Umar alifika kwenye utawala kwa njia ya kuteuliwa na Khalifa Abu Bakr, na Khalifa Uthman alifika kwenye utawala kwa njia ya kupewa kiapo cha utii na watu sita kati ya Masahaba aliowateua Umar katika kisa cha Shura maarufu, lakini Imam Ali (as) alifika kwa njia nyingine tofauti, na hiyo ni kwamba watu wa Ummah walisongamana kwake na wakamuomba achukue ukhalifa kama alivyosema (as) katika kauli iliyopokewa kutoka kwake:

**فَمَا رَاعَنِي إِلاَّ وَالنَّاسُ كَعُرْفِ الضَّبُعِ إِلَيَّ, يَنْثَالُونَ عَلَيَّ مِنْ كُلِّ جَانِبٍ، حَتَّى لَقَدْ وُطِىءَ الْحَسَنَانِ، وَشُقَّ عِطْفَايَ، مُجْتَمِعِينَ حَوْلِي كَرَبِيضَةِ الغَنَمِ.**

**"Nilishitushwa na kundi la watu likimiminika kuja kwangu mfano wa manyoya ya shingoni mwa fisi toka kila upande, kiasi kwamba Hasan na Husein walikanyagwa, na sehemu za ncha za mabega ya vazi langu zikararuriwa, watu hao walijikusanya kunizunguka kama kundi la kondoo na mbuzi."[22]**

[22] Nahjul-Balaghah khutuba ya 3

Imekuja katika Tarikh Tabariy: Kutoka kwa Abi Bashiri al-'Abidiy amesema:

"Nilikuwa Madina wakati wa kuuliwa Uthman (r.a) Muhajirina na Answar wakakusanyika akiwemo Talha na Zubeir, wakamwendea Ali na kumwambia: 'Ewe Abu Hasan njoo tukupe kiapo cha utii.' Akasema: 'Sina haja na uongozi wenu, mimi niko pamoja nanyi, mtakayemchagua nitamridhia, chagueni.' Wakasema: 'Wallahi hatuchagui asiyekuwa wewe.' Anasema: Wakasongamana kwake kwa wingi baada ya kuuliwa Uthman (r.a)"[23]

Tabariy ametaja zaidi ya riwaya moja zinazotia mkazo madhumuni haya na kwamba Ali (as) alikuwa anawaambia kwamba kama yeye atachukua ukhalifa atatekeleza mfumo wake katika kuleta marekebisho, kama vile kauli yake (as): "Na jueni hakika mimi kama nitawakubalia nitawaongoza kwa ninayoyajua."[24]

Na ni maarufu kihistoria kwamba katika zama za Khalifa Uthman bin Affan kulitokea hali ambayo Masahaba wengi hawakuipenda na hawakuiridhia, na sehemu kubwa zaidi ya Ummah ilikuwa imeudhika nayo, kwa sababu wasaidizi waliomzunguka Khalifa miongoni mwa jamaa zake ambao alikuwa anawaamini. Hawa walitumia vibaya imani ya Khalifa kwao, na sasa hivi hatuko mahala pa kuelezea kwa ufafanuzi kwani hayo yamo ndani ya vitabu vya historia na katika utafiti mzuri wa kimaudhui, utafiti ambao ameuandika Sheikh Abul-A'alaa al-Maudud, mwanachuoni maarufu mwanzilishi wa Jama'atul-Islamiya huko Pakistan, na aliyepata tuzo ya Mfalme Faisal ya ulimwengu ya kuutumikia Uislamu mwaka 1979, na kitabu chake kimekuja chini ya anwani *al-Khilafatu Wal-Mulku*[25]

[23] Nahjul-Balaghah khutuba ya 3
[24] Twabariy: Muhammad bin Jarir katika *Tarikhul-Umami wal-Muluuki*, Juz. 3, uk: 450 Muasastu al- ilimiy chapa 5 ya 1989, Beirut.
[25] Rejea iliyotangulia uk. 456

nacho kimechapishwa zaidi ya mara moja. Humo amezungumzia mabadiliko ambayo yalitokea katika hali ya Ummah katika zama ya Khalifa Uthman, ambapo alikwenda mbali na mfumo wa Nabii na mfumo wa ukhalifa wema, pakawa na desturi ya kuchezea mali na ubadhirifu kutoka kwa wasaidizi wake, jambo ambalo lilikuwa ni moja ya sababu iliyoleta hali ya ghadhabu ndani ya watu na Ummah, ghadhabu ambayo ilimalizika kwa kushambuliwa nyumba ya Khalifa na kumuuwa kwa sura mbaya, jambo ambalo liliimarisha hali ya mabavu ya kisiasa katika historia ya Ummah.

Baada ya hayo ndipo akaja katika uongozi Amirul-Muuminina Ali bin Abu Talib (as), akapendekeza mfumo wake wa urekebishaji, na tusisahau kwamba Imam alielezwa yeye awe Khalifa baada ya kuuliwa Khalifa Umar lakini kwa sharti apokonywe uhuru wake katika urekebishaji na mageuzi chini ya anwani ya kujilazimisha na sira ya Masheikh Wawili. Ali (as) alikataa ukhalifa kwa sharti hili lakini Uthman alikubali sharti hili. Haya yameandikwa na vitabu vya historia, ambapo walikusanyika Masahaba sita kwa ajili ya Shura, Masahaba ambao aliwateua Umar baada ya kujeruhiwa kwake, nao walikuwa ni Talha, Zubeir, Saad bin Abi Waqaas, Abdurahman bin Auf, Uthman bin Affan na Ali bin Abu Talib. Na uongozi na uenyekiti wa kuendesha kikao ulikuwa ni wa Abdurahaman bin Auf ambaye alimgeukia Ali bin Abu Talib kwa kusema: “Je, wewe Ali utakubali kiapo cha utii kwa sharti la kutenda kwa mujibu wa Kitabu cha Mwenyezi Mungu, Sunnah ya Nabii Wake na sira ya Abu Bakr na Umar?” Ali akasema hapana, lakini kwa ijtihad yangu katika hilo na uwezo wangu. Hiyo ni kulingana na alivyotaja Tabariy.[26]

Ibnu Athir ametaja: Kwamba Abdurahman bin Auf alimwita Ali na akamwambia: “Ni juu yako ahadi ya Mwenyezi Mungu na mafungamano yake utahukumu kwa Kitabu cha Mwenyezi Mungu na

[26] Twabariy: Muhammad bin Jarir juzuu 3 uk: 301

Sunna ya Mtume Wake na sira ya Masheikh Wawili baada yake." Ali akasema: "Nataraji nitafanya kwa upeo wa elimu yangu na uwezo wangu."[27] Ibnu Auf akamwelekea kumpa kiapo cha utii Uthman bin Affan ambaye alikubali sharti hili na wala hakulihifadhi. Na ameelezea msimamo huu mwanaharakati wa Kiislamu wa Kuwait Dr. Ismail Shatwiy, akiashiria kwenye nukta muhimu ambapo amesema ndani ya makala yake: "Kizazi cha mwanzo cha Waislamu (r.a) kilikaribia kuufanya uzoefu wake wa kisiasa na kiutawala katika uendeshaji wa dola kuwa ni sehemu ya sharia kama sio Ali bin Abu Talib, Mwenyezi Mungu autukuze uso wake, kupambana na kuzuia jaribio hili, na mapambano haya yalimgharimu gharama ambayo ni kupoteza nafasi ya ukhalifa baada tu ya kutangaziwa kupewa ukhalifa huo, pale alipokataa kujilazimisha na uzoefu wa Masheikh Wawili baada ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Nabii wake. Ambapo tathmini yake ilionesha kwamba uzoefu huu (wa Masheikh Wawili) haukuwa chochote isipokuwa ni ijtihadi binafsi ya kibinadamu ambayo itapanuka baada yao na kufika katika upeo mkubwa wa mustakabali mpana (na hatimaye watu wataufanya ni sharia ya Mungu ilihali ni matakwa ya mtu binafsi). Na kwa kujitolea kwake huku Imam alisimamisha – Mwenyezi Mungu autukuze uso wake - mwenendo uliokomaa katika dini hadi katika mpaka wa nyanja hizo."[28]

**Kujitolea kwa ajili ya Urekebishaji:**

Imam Ali alipochukua ukhalifa alianza kutekeleza mfumo wake wa urekebishaji, pamoja na kujua kwake vikwazo vikubwa na vizin-

[27] Ibnu Al- Athiyr: Katika *al-Kaamil fiy Taarikh*, Juz. 2, uk. 223 Muasastu al-Arabiy chapa 1 mwaka 1989 Beirut

[28] Shatwiy: Dr. Ismail katika *al-Islaamu Alladhiy Nuriid*, Jarida la Sharqi al- ausat tolea la 7131 tarehe 7/6/ 1998

giti vingi ambavyo vitamkabili, kama alivyosema alipokuwa anatoa sababu inayomfanya yeye akatae ukhalifa:

**دَعُونـي وَالْتَمِسُوا غَيْرِي, فإِنَّا مُسْتَقْبِلُونَ أَمْراً لَهُ وُجُوهٌ وَأَلْوَانٌ; لاَ تَقُومُ لَهُ الْقُلُوبُ، وَلاَ تَثْبُتُ عَلَيْهِ الْعُقُولُ، وَإِنَّ الاْفَاقَ قَدْ أَغَامَتْ، وَالْمَحَجَّةَ قَدْ تَنَكَّرَتْ. وَاعْلَمُوا أَنِّي إنْ أَجَبْتُكُمْ رَكِبْتُ بِكُمْ مَا أَعْلَمُ، وَلَمْ أُصْغِ إِلَى قَوْلِ الْقَائِلِ وَعَتْبِ الْعَاتِبِ، وَإِنْ تَرَكْتُمُونِـي فَأَنَا كَأَحَدِكُمْ; وَلَعَلِّي أَسْمَعُكُمْ وَأَطْوَعُكُمْ لِمنْ وَلَّيْتُمُوهُ أَمْرَكُمْ، وَأَنَا لَكُمْ وَزِيراً، خَيْرٌ لَكُمْ مِنِّي أَمِيراً.**

**"Niacheni na tafuteni mtu mwingine, kwa kuwa sisi twatazamia jambo lenye sura nyingi na rangi nyingi. Nyoyo haziwezi kuvumilia wala akili haziwezi kulibeba. Kwa kweli msitari wa upeo wa macho umefunikwa na mawingu, na njia iliyonyooka haijulikani tena. Na jueni kwamba endapo mimi nitawaitikieni nitawabebesheni niyajuayo na sitosikiliza kauli ya msemaji yoyote, wala lawama ya mwenye kulaumu. Na mkiniacha (msiponipa kiapo chenu cha utii) mimi nitakuwa kama mmoja yeyote miongoni mwenu. Na huenda nitakuwa mwenye kumsikiliza na kumtii sana mtakayemtawalisha hili suala lenu, na mimi kuwa waziri kwenu ni bora kuliko kuwa amiri."**[29]

Na hapa tunakuta ni lazima iwepo nukta ya kwanza ya utendaji wa kazi ya urekebishaji nayo ni kujitolea na kupambana. Wengi wa-

[29] Nahjul-Balaghah khutuba ya 92

naweza kubeba nembo ya urekebishaji na wanaweza kuipendekeza kinadharia. Na kuna wengi kati ya watu wanaujua urekebishaji kwa ajili ya kubadilisha hali yao na kwenda kwenye ubora, lakini kuanza urekebishaji kunahitaji kujitolea na kupambana. Na uongozi wa kidini na kisiasa ndio unaobeba majukumu haya kwa daraja la kwanza, nao ndio wanaoweza kuyatekeleza kutokana na kumiliki hatamu za mambo na kutokana na nafasi ya kuathiri, kushawishi na kutekeleza waliyonayo katika Ummah.

Hakika kazi yoyote ya urekebishaji inahitaji kujitoa muhanga na gharama, na inakabiliwa na ugumu na vikwazo, lakini kupambana kwa viongozi kunafanya kazi iwe na ugumu mchache na karibu zaidi na mafanikio. Ama kama mambo yataachwa yaende kwa vitendo vya kisasi na ghadhabu zilizomo katika nafsi za watu, hali inaweza kulipuka na kutoka katika udhibiti, na watakabiliana nayo wasio na uwezo na wasio na ikhilasi, na hatimaye maadui wa Ummah watapata fursa yao ya kufanya ufisadi na uharibifu.

Na katika sira ya Imam Ali (as) na sira ya Khalifa Umar bin Abdul Aziz kuna vyanzo vya maarifa na mafunzo ya kuiga, licha ya kwamba baina ya shakhisiya hizi mbili kuna tafauti isiyofichikana, katika upande wa nafasi, sifa, hali na mazingira.

Hakika uchaguzi bora mbele ya wananchi wa Ummah wa Kiislamu leo, utakaowafanya watoke katika matatizo na kuvuka hali ya kutokuendelea, ni kujitolea kwa ujasiri kwa viongozi wa kisiasa wenye kutawala na kuelekea upande wa urekebishaji kwa kuwa wawazi mbele ya wananchi, na kupanua ushirikiano wa kisiasa na kutegemea mfumo wa haki na uadilifu. Kama ambavyo ni juu ya viongozi na Marjaa wa kidini kudhihirisha misimamo ya haki na wala wasiwe wapole mbele ya pande zenye kuufanyia ubaya Uislamu, na

kukhalifu misingi yake na maadili yake. Na wajitolee kurekebisha katika kiwango cha kifikra na kiutamaduni.

## Mipango ya Urekebishaji:

Imam Ali (as) alishajitolea tangu mwanzo wa utawala wake kutekeleza mpango wa urekebishaji, akawauzulu magavana wasio wema katika uongozi, ambao walichukua nafasi zao katika uzani wa chumo na wakahodhi mamlaka na utajiri wa Ummah. Kama ambavyo alirudisha mali za Baitul-Mali kutoka katika mikono ya wenye hiyana ambao walijihodhi mali hizo kwa njia zisizo za kisharia, na hakukubali kufumbia macho hilo, bali aliwajibu wapinzani kwa kauli yake: "Wallahi hata kama nitakuta mtu ameolea mke mali hiyo na amemiliki kwayo kijakazi, nitairudisha. Hakika uadilifu ni mpana, na ambaye uadilifu kwake ni mfinyu basi dhulma kwake ni finyu zaidi."[30]

Na akaweka uangalizi kwa magavana na watumishi na akatumia ukali panapotokea upotovu au ukiukwaji wa sharia kutoka kwa yeyote kati yao.

Na ilikuwa miongoni mwa mpango wake muhimu sana wa urekebishaji ni kutekeleza uadilifu na usawa baina ya watu katika kuwapa, baada ya kuwa watu walikabiliwa na ubaguzi baina yao, jambo ambalo lilikuza hali ya matabaka na kuukusanya utajiri katika tabaka moja, na kuongeza ufakiri kwa matabaka yaliyobakia. Alikabiliwa na upinzani mkubwa lakini yeye alisimama thabiti mbele yake na akashikamana na mfumo wake wa uadilifu na usawa. Alikuwa mkali katika nyuso za wapinzani:

[30] Nahjul-Balaghah, khutuba ya 15

أَتَأْمُرُونِّي أَنْ أَطْلُبَ النَّصْرَ بِالْجَوْرِ فِيمَنْ وُلِّيتُ عَلَيْهِ! وَاللهِ لاَ أَطُورُ بِهِ مَا سَمَرَ سَمِيرٌ، وَمَا أَمَّ نَجْمٌ فِي السَّمَاءِ نَجْماً! لَوْ كَانَ الْمَالُ لِي لَسَوَّيْتُ بَيْنَهُمْ، فَكَيْفَ وَإِنَّمَا الْمَالُ مَالُ اللهِ لَهُمْ.

**"Mnaniamrisha niombe usaidizi kwa kuwadhulumu ambao nimetawazwa juu yao. Naapa kwa Mwenyezi Mungu! Katu sitofanya hivyo kadiri dunia iendeleavyo kuwepo, na kwa kadiri nyota moja mbinguni iiongozavyo nyota nyingine. Hata mali ingekuwa yangu ningewagawia kwa usawa, basi hali itakuwaje ikiwa mali ni ya Mwenyezi Mungu!"[31]**

## Utamaduni wa Mageuzi na Urekebishaji:

Ili mpango wa urekebishaji ufuate njia yake katika medani ya Ummah ni lazima kuwe na utamaduni wa kuunga mkono na kushajiisha watu kuvuka na kuacha yale waliyoyazoea miongoni mwa ada mbaya na fikra zisizo sahihi, na kuacha kuzikumbatia kutokana na kuathirika na vituo vya nguvu zilizo dhidi ya kazi ya urekebishaji, na kutengeneza mazingira yanayofaa kwa ajili ya mabadiliko.

Na hii ndio hali ambayo alikabiliana nayo Amirul-Muumina Ali (as) katika mwelekeo wa utawala wake, ambapo alirudia maamuzi yake ya urekebishaji kwa mashambulizi ya kiutamaduni, ili kuhuisha misingi ya uadilifu na urekebishaji katika nyoyo za watu, na ili kukabiliana na makundi ya ufisadi na upotovu. Yeye (as) alifanya jukumu lake kama Khalifa, na kama kiongozi na Imamu muongozaji pia.

[31] Nahjul-Balaghah, khutuba ya 126

Kwa sababu hiyo hazina ya kifikra na maarifa ya Ali (as) yalikuwa ni yenye kuonekana na ya kipekee kabisa kwa idadi na namna ukilinganisha na Makhalifa wengine, ambapo rejea zimenukuu idadi kubwa miongoni mwa hotuba ambazo alizitoa kwa watu, na risala ambazo alizituma kwa magavana wake na watumishi wake, na hotuba ambazo aliwahutubia kwazo wafuasi wake na walio karibu yake.

Sharif Ridhaa (r.m) amekusanya sehemu ya maneno ya Amirul-Muuminina Ali (as) katika kitabu chake mashuhuri *Nahjul-Balaghah*. Amekusanya hotuba 239, risala 79 ukiongezea na idadi kubwa ya maneno mafupi, lakini hayawakilishi isipokuwa sehemu tu ya hazina ya Imam. Na amejitolea mmoja wa Maulamaa wahakiki wa kileo naye ni Sheikh Muhammad Baqir al- Mahamuudiy (aliyezaliwa mwaka 1341 na kufariki mwaka 1327 Hijiria) kukusanya hotuba zingine za Imamu na risala zake na wasia wake, basi zikawa ni nyingi kuliko zilizokusanywa katika *Nahjul-Balaghah,* na rejea hii imechapishwa katika juzuu nane chini ya anwani ya *Nahju Sa'adat Fiy Mustadraki Nahjul-Balaghah*, rejea hii imekusanya hotuba 409, risala 185 wasia 65 na dua 105.

Na katika mambo ambayo yanaashiria juhudi hii ya kimaarifa ya kiutamaduni ambayo ameitoa Imam Ali (as) katika zama za ukhalifa wake - pamoja na ufupi wake – ni yale ambayo ameyataja mwanahistoria al-Masuudiy (aliyefariki mwaka 346 Hijiria) katika *Muruujud-Dhahab* ambapo amesema: "Na ambayo watu wameyahifadhi kutoka kwake miongoni mwa hotuba zake mbalimbali ni hotuba mia nne thamanini na zaidi."[32] Na amenukuu mfano wa hayo Ahmad bin Is'haq al-Yaqubiy (ambaye ni mmoja kati ya Maulamaa wa karne ya tatu Hijiria) katika kitabu chake *Mishakilatun-Naasi Lizamaanihim*, amesema: "Watu wamehifadhi kutoka kwake hotuba mbalimbali,

[32] Al-Masuudiy: Ali bin Husain katika *Muruuju -Dhahabi* Jz. 2, uk. 419 Darul Hijira chapa ya pili 1984 Qum

hakika alihutubia hotuba mia nne ambazo zimehifadhiwa kutoka kwake, nazo ndio zinazozunguka baina ya watu na wanazitumia katika hotuba zao na maneno yao."[33]

Hizi ni baadhi tu ya dondoo za waandishi juu ya uzoefu wa Ali (as) na sira yake katika urekebishaji na mageuzi, uzoefu huo ambao umembebesha taabu nyingi, ambapo aliingia katika vita tatu kali; vita ya Jamali, Sifin na Nahrawan, na asingeweza yeyote asiyekuwa Ali (as) kuthubutu mbele ya kibano kikubwa na upinzani mkali, kwa ajili ya kuupa Ummah na vizazi uzoefu bora katika harakati za urekebishaji na kusimamisha utawala adilifu mwema kama alivyosema (as):

**أَيُّهَا النَّاسُ فَإِنِّي فَقَأْتُ عَيْنَ الْفِتْنَةِ، وَلَمْ يَكُنْ لِيَجْتَرِىءَ عَلَيْهَا أَحَدٌ غَيْرِي بَعْدَ أَنْ مَاجَ غَيْهَبُهَا، وَاشْتَدَّ كَلَبُهَا.**

**"Kwa hakika mimi nimelitoboa jicho la fitina (nimeishinda), na hangethubutu mwingine yoyote asiyekuwa mimi baada ya kutanda giza (upotofu) lake, shari yake, na maudhi yake kuwa makali."[34]**

Na akatoa uhai wake kama thamani ya mfumo huu wa urekebishaji ambapo alifariki shahidi katika mihrabu ya Swala yake. Amani iwe kwake siku aliyozaliwa na siku aliyokufa shahidi na siku ya kufufuliwa.

[33] Al-Yaaqubiy: Ahmad bin Is'haq katika *Mashakilatun-Naasi Lizamaanihim* uk. 15 Darul kutubi ali jaded chapa ya 1 mwaka 1962 Beirut.

[34] Nahjul-Balaghah, khutuba ya 92

# IMA UREKEBISHAJI WA JUMLA AU MLIPUKO WA NDANI[35]

Amesema Sheikh Hasan Safar kwamba Ummah uko njiapanda na ni lazima uvuke kikwazo kinachozuia mabadiliko, hivyo ni wajibu kujitolea kufanya marekebisho makubwa, vinginevyo matatizo yataongezeka na majanga yatazidi, hali ambayo inaweza kuulipua Ummah kwa ndani.

Na ameongeza as-Safar kwa kusema katika muhadhara wake uliozungumzia urekebishaji wa kisiasa wa Imam Ali (as), alioutoa usiku wa ijumaa katika kumbukumbu ya kifo cha kishahidi cha Imam Ali (as), kwamba ni juu ya viongozi wakuu wa Ummah wa kisiasa na wa kidini kubeba majukumu yao mukabala na hali ilipofikia.

Na Safar amerudia kukumbusha umuhimu wa kumsoma Imam Ali upya kwa namna itakayotusaidia kutatua matatizo yetu yaliyopo na kuchukua mazingatio, na sio kwa namna itakayozidi kutuingiza katika matatizo yaliyopita ya kihistoria. Na amesisitiza umuhimu wa kufanya marejeo, kwa kuwepo uwezekano wa kuwepo makosa yenye kuendelea kwa wote, au kuwepo upotovu wa kudhamiriwa au kutokudhamiriwa, na mwisho ni kwa sababu ya tabia ya mabadiliko na mahitajio ya mazingira ya leo.

Na ameongeza kwamba inawezekana hali ya kutokuendelea iliyopo katika nchi zetu nyingi inatokana na kuwepo utamaduni unaozuia mabadiliko, na kuwepo nguvu za maslahi mbalimbali zinazoogopa kupoteza na kukosa maslahi yake.

Safar amehadharisha uwezekano wa kujitokeza majanga na matatizo zaidi ikiwa viongozi wa Ummah wa kisiasa na wa kidini

[35] Umesambazwa katika tovuti Raswid al- ikhibariya tarehe 13/ 10/ 2006

hawatajitolea kwa ajili ya marekebisho makubwa, hivyo ugaidi wa kidini, ufakiri, kutokuendelea kwa ndani, mkanganyiko wa kufarakanisha, vita vya nje na vya makundi, ni mambo yanayoweza kushamiri.

Na kuhusu sababu zinazoweza kusaidia kurekebisha, Safar ameona kwamba sisi tuna haja ya kumiliki ujasiri na subira mbele ya tuhuma, sambamba na kusambaza utamaduni wa urekebishaji baina ya watu, na mwisho ni uelewa wa watu utakaosaidia kuleta marekebisho. Na amesema hakika nchi yetu kama zilivyo nchi nyingine nyingi inakabiliwa na ufisadi wa kiidara, na kwamba jukumu la kurekebisha hilo halirejei kwa mtawala peke yake, bali ni letu sote. Sote tunakusudiwa na ni wenye jukumu la kufichua mchezo mchafu na ufisadi na kufikisha hayo katika kiwango cha juu.

Na ameongeza kwamba harakati hizi zinatakiwa katika viwango vipya kwa kuanzia na imamu wa jamaa, kiongozi wa klabu, jumuiya, kiongozi wa serikali hadi kufikia kwa Marjaa wa taqlid. Ni lazima kila mmoja kati yetu awe na msimamo dhahiri na wa wazi katika ukosoaji na kutoa upinzani kwa njia za hekima kwa ajili ya kutumikia jamii, dini na nchi, Safar aliongezea.

Alitilia mkazo suala la kuiga sira ya Imam Ali ya urekebishaji kabla na baada ya kufika kwake katika utawala kwa kuungwa mkono na watu kwa wingi baada ya hapo mwanzo kukataa kuchukua utawala chini ya sharti la kujilazimsha kufuata ijtihadi ya Makhalifa waliomtangulia. Ali alijitolea kufanya marekebisho ya jumla kwa kuwauzulu magavana wasioridhiwa na kufuta siasa ya ubaguzi katika kutoa baina ya Waislamu, na kufuta upendeleo, na kwa ajili hiyo walitoka dhidi yake wale wenye maslahi, Safar alimalizia.

Na maneno ya Sheikh Safar yamekuja katika semina ya Ali na Ummah ambayo imeandaliwa na kitengo cha Imam Hasan katika

kiwanja cha Shawikah huko Qatif, na ilihudhuriwa na watu wengi miongoni mwa wananchi na itamalizika usiku wa leo.

Na mazungumzo ya Sheikh Safar yalitanguliwa na mashairi kuhusu Imam Ali (a.s.), ya mshairi Habib al-Ma'atiyq ambaye alisoma kaswida iliyozungumzia harakati za watu, na ambapo mshairi Farid Nimri alianza ratiba ya usiku uliopita kwa kaswida inayofanana na hiyo.

# KUENDELEZA UBINADAMU KATIKA ZAMA ZA IMAMU ALI (AS)

Tunaposoma sira ya Amirul-Muuminina Ali (as) wakati wa kushika kwake utawala na ukhalifa, na kutafakari risala zake kwa magavana na watumishi, na hotuba zake kwa watu, tunakuta kwamba alikuwa anajali kuboresha maisha ya watu wa Ummah na kuwaendeleza katika nyanja mbalimbali, na kulingana na msemo wa kileo alikuwa anajali kumwendeleza binadamu na hakuwa tu ni kiongozi wa kidini anayejali kueneza itikadi na kutekeleza sharia tu, na hakuwa ni mtawala wa kisiasa anayejali kuimarisha uongozi wake na utawala wake tu, bali alikuwa ni mwenye mkakati wa kimaendeleo unaolenga kumboresha mwanadamu na kuibua vipaji vyake na uwezo wake ili aneemeke kwa maisha matukufu na kuelekea kwenye harakati za uwazi, na hilo ndio lengo la msingi la itikadi na sharia.

Katika upande wa maendeleo ya kisiasa Imam Ali (as) anashajiisha watu kudhihirisha rai zao za kisiasa na wala wasisite katika kupinga kosa lolote mbele ya mtawala, na wala wasiamiliane pamoja na mtawala kwa mantiki ya unyonge na woga anasema (as):

فَلاَ تُكَلِّمُونِي بِمَا تُكَلَّمُ بِهِ الْجَبَابِرَةُ، وَلاَ تَتَحَفَّظُوا مِنِّي بِمَا
يُتَحَفَّظُ بِهِ عِنْدَ أَهْلِ الْبَادِرَةِ، وَلاَ تُخَالِطُونِي بِالْمُصَانَعَةِ، وَلاَ
تَظُنّوا بِيَ اسْتِثْقَالاً فِي حَقٍّ قِيلَ لِي، وَلاَ الْتِمَاسَ إِعْظَام
لِنَفْسِي.فَإِنَّهُ مَنِ اسْتَثْقَلَ الْحَقَّ أَنْ يُقَالَ لَهُ أَوْ الْعَدْلَ أَنْ

يُعْرَضَ عَلَيْهِ، كَانَ الْعَمَلُ بِهِمَا أَثْقَلَ عَلَيْهِ. فَلاَ تَكُفُّوا عَنْ مَقَالَةٍ بِحَقٍّ، أَوْ مَشُورَةٍ بِعَدْلٍ، فَإِنِّي لَسْتُ فِي نَفْسِي بِفَوْقِ أَنْ أُخْطِىءَ، وَلاَ آمَنُ ذلِكَ مِنْ فِعْلِي.إِلاَّ أَنْ يَكْفِيَ اللهُ مِنْ نَفْسِي مَا هُوَ أَمْلَكُ بِهِ مِنِّي.

**"Wala msinisemeshe kama mnavyo wasemesha madhalimu, (kuwasifu madhalimu kwa sifa wasizo nazo) wala msijilinde mbele yangu kama mnavyojilinda mbele ya wenye ghadhabu, wala msiwe pamoja nami kwa kujipendekeza, wala msinidhanie kwamba nakuwa mzito niambiwapo haki, wala si mwenye kutaka kujitukuza binafsi. Kwani mwenye kuwa mzito aambiwapo ukweli, au uadilifu awekewapo mbele yake, kutenda mawili hayo atakuwa mzito mno. Hivyo basi msijizuwiye kusema ukweli, au kutoa ushauri wa kiadilifu, kwa kuwa mimi nafsini mwangu sijichukui kuwa niko juu ya kukosea, wala sijiaminishi hayo katika matendo yangu, isipokuwa kama Mwenyezi Mungu ataitosheleza nafsi yangu ambalo Yeye ni mwenye uwezo wa kuimiliki zaidi kuliko mimi."[36]**

Imam alitangaza mbele ya watu kuwa atalinda haki ya upinzani na kutowabana kijamii na kiuchumi. Wala hatotumia mabavu dhidi yao maadamu upinzani wao ni wa amani na hawakutumia humo silaha. Imekuja katika *Daaimul-Islam* kwamba siku moja alihutubia huko Kufah na mara akasimama mwanaume kati ya Makhawariji akasema: "Hakuna hukumu isipokuwa ya Mwenyezi Mungu." Ali alinyamaza, kisha akasema mwingine na mwingine tena maneno hayo hayo, walipozidisha kwake akasema (as): "Neno la haki inakusudiwa humo batili, mnayo mambo matatu kwetu: Hatuwazuii kuja

[36] Nahjul-Balaghah, khutuba ya 207

msikitini na kuswali humo, wala hatuwanyimi pato maadamu mikono yenu ipo pamoja na mikono yetu wala hatutowaanza kwa vita hadi mtuanze."[37]

Katika upande wa kukuza uchumi na kuwapatia mahitaji wananchi, tunakuta tamko limenukuliwa katika zaidi ya rejea moja za kihistoria kwamba Ali (as) aliwahutubia watu wa Kufah kwa kusema: "Hajaamka yeyote Kufah isipokuwa ni tajiri - yaani ameneemeka – hakika mwenye nafasi ya chini anakula ngano na anakaa katika kivuli – ana nyumba – na anakunywa maji ya furati."[38] – Na Kufah wakati huo ulikuwa ni mji mkubwa wenye wakazi wengi na makabila tofauti tofauti, unatembelewa na watu kutoka miji mbalimbali na kutoka sehemu mbalimbali, humo kuna waarabu toka makabila mbalimbali na kuna waajemi, humo kuna maaskari na kuna raia, na humo kuna aina mbalimbali za watu na mielekeo yao ni mbalimbali kifikira, na humo kuna anayempenda Ali (as) na kuna anayemchukia.

Amesema Sayyid Husain al-Baraqiy (aliyefariki mwaka 1322 Hijiria) katika kitabu chake *Tarikhul-Kufah*: "Kufah ilikuwa pana na kubwa, vijiji vyake na viunga vyake vinafika hadi Furati ya asili na vijiji vya al-Adhaariy, inafikia maili 16 na thuluthi mbili, amesema Yaaqut katika kumusi yake: 'Imetajwa kwamba humo kulikuwa kuna nyumba elfu hamsini za waarabu kutoka kabila la Rabi'atu na Mudhar, na ishirini na nne elfu za waarabu wengine, na elfu sita ni nyumba za wayemeni.'"[39]

Pamoja na aina hii anasema (as): "Hajaamka Kufah yeyote isipokuwa tajiri," yaani anaishi katika neema na ananeemeka kwa

[37] Al- Baraaqiy: Husain katika *Tarikhul-Kufah*, uk. 134 chapa ya 21960, chapa ya Haidariya Najaf tukufu.

[38] Al- Majilisiy: Muhammad Baaqir katikaBiharul- Anwaar, Juz. 40, uk. 327 chapa 3 mwaka 1403 Daru ihiyaai turath al- arabiyi Beirut

[39] Al- Baraaqiy: Husain katika Tarikhul-Kufah, uk. 134 chapa ya 21960, chapa ya Haidariya Najaf tukufu.

neema, au neema kwa maana ya raha. Na hii ina maana kwamba kila mkazi wa Kufah sawa awe ni kati ya watu wake na wenyeji wake au mgeni na mhamiaji, wote walineemeka kwa neema. Kisha anasema: "Hakika mwenye nafasi ya chini," mwenye kiwango cha chini katika maisha katika watu wa Kufah "Anakula ngano" na hii inamaana kwamba hakuna mwenye njaa Kufah, mtu wa hali ya chini kabisa kijamii na kiuchumi kinapatikana kwake chakula cha kutosha, "na anakaa katika kivuli" anamiliki nyumba ya kujihifadhia. Chakula na makazi yanapatikana kwa kila mtu, na vile vile maji "Na anakunywa katika maji ya Furati."

Na tamko hili linaungwa mkono. Imekuja katika nususi nyingine kwamba mzee mmoja kipofu mkubwa kwa umri alipita huku akiwa anaomba, Amirul-Muuminina akasema: "Ni nani huyu?" Wakasema: "Ewe Amirul-Muuminina ni mnaswara!" Amirul-Muuminina (as) akasema: "Mmemtumia hadi alipozeeka na akawa kikongwe ndipo mnamnyima? Mpeni kutoka Baitul-Mali."[40]

Hakuna tofauti kwa Amirul-Muuminina Ali bin Abu Talib (as) baina ya kuwa huyu mtu ni mwislamu au mnaswara, ni wajibu kupatikane kwa kila mtu njia na mahitaji ya maisha mazuri na mahitaji yake ya msingi. Imepokewa kwamba: Waliingia watu kwa Amirul-Muuminina (as) siku moja kabla ya kufa kwake shahidi na wakashuhudia wote kwamba ameshawapa fungu lao na amewaachia dunia yao na hakuchukua rushwa katika kutoa hukumu zao na wala hajachukua katika Baitul- Mali yaliyo sawa na egali, na wala hajala katika mali yake isipokuwa kwa kiasi kidogo, na wakashuhudia wote kwamba mtu wa chini sana kwa daraja kwake ndiye mtu wa karibu sana naye.[41]Imam Ali (as) alikuwa anabeba huzuni na hima

[40] Tuusiy: Muhammad bin Hasan katika Tahadhibul- Ahkaami, Juz. 6, uk. 292 Hadith namba 811 chapa 2 Darul kutubil- Islamiya Najaf.

[41] Sheikh Mufid katika kitabu al- ikhitiswaasi, uk. 160 chapa 1425 Hijiria muasasatu Nashiril- Islamiy Qum

ya uwezekano wa kuwepo fakiri katika sehemu ya mbali na makazi yake, anasema:

وَلَوْ شِئْتُ لاَهْتَدَيْتُ الطَّرِيقَ، إِلَى مُصَفَّى هذَا الْعَسَلِ، وَلُبَابِ هذَا الْقَمْحِ، وَنَسَائِجِ هذَا الْقَزِّ، وَلكِنْ هَيْهَاتَ أَنْ يَغْلِبَنِي هَوَايَ، وَيَقُودَنِي جَشَعِي إِلَى تَخَيُّرِ الْأَطْعِمَةِ ـ وَلَعَلَّ بِالْحِجَازِ أَوِ الْيَمَامَةِ مَنْ لاَطَمَعَ لَهُ فِي الْقُرْصِ، وَلاَ عَهْدَ لَهُ بِالشِّبَعِ

**"Lau ningependa ningeongoka njia ya kwenye asali hii safi, na ngano hii safi, na nguo ya hariri. Lakini niko mbali sana kutokana na kuhadaliwa na utashi mbaya wa nafsi yangu, na kusukumwa na uroho wangu kwenye kuchagua vyakula. Na huenda huko Hijazi au al-Yamama kuna ambaye hana matumaini ya kupata mkate, wala hana mazoea ya kushiba."** [42]

## MIFUMO YA KUENDELEZA:

Na tunaweza kuona kwamba malengo ya Imam katika kuhakikisha anamwendeleza mwanadamu katika nyanja zake mbalimbali, yalikuwa yanategemea mifumo mitatu:

**Kwanza:** Kuwaamsha watu ili wafanye wajibu wao katika maisha na ili waibue vipaji vyao vilivyofichikana na wawe na matarajio na lengo kubwa. Na katika yaliyonukuliwa kutoka katika maneno ya Ali (as) katika *Nahjul-Balaghah* na mengineyo kati ya rejea ni utajiri mkubwa katika nyanja hii.

[42] Nahjul-Balaghah, barua 45

**Pili:** Kuwalingania watu kushirikiana baina yao na kwa ajili ya kujitolea kwa baadhi kuwahudumia baadhi yao, na kujali sehemu za udhaifu na zenye kuhitajia katika jamii, lile ambalo hivi sasa linajulikana kama kazi ya kujitolea ya kuhudumia jamii, alisisitiza hilo kama vile ilivyo katika kauli yake (as) katika wasia wake kwa Hasan na Husain:

**أُوصِيكُمَا بِتَقْوَى اللّٰهِ، وأَلَّا تَبْغِيَا الدُّنْيَا وَإِنْ بَغَتْكُمَا، وَلاَ تَأْسَفَا عَلَى شَيْءٍ مِنْهَا زُوِيَ عَنْكُمَا، وَقُولاَ بِالْحَقِّ، وَاعْمَلاَ لِلْأَجْرِ، وَكُونَا لِلظَّالِمِ خَصْماً، وَلِلْمَظْلُومِ عَوْناً. أُوصِيكُمَا، وَجَمِيعَ وَلَدِي وَأَهْلِي وَمَنْ بَلَغَهُ كِتَابِي، بِتَقْوَى اللّٰهِ، وَنَظْمِ أَمْرِكُمْ، وَصَلاَحِ ذَاتِ بَيْنِكُمْ، فَإِنِّي سَمِعْتُ جَدَّكُمَا ـ صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ـ يَقُولُ: "صَلاَحُ ذَاتِ الْبَيْنِ أَفْضَلُ مِنْ عَامَّةِ الصَّلاَةِ الصِّيَامِ."**

**"Nakuusieni kumcha Mwenyezi Mungu, na msiitake dunia japo itakutakeni, wala msikihuzunikie kitu kilichochukuliwa na mkanyimwa. Semeni kweli, na tendeni kwa ajili ya ujira wa kesho (wa Siku ya Kiyama), na kuweni mahasimu kwa madhalimu na wasaidizi kwa mwenye kudhulumiwa. Nakuusieni nyinyi wawili na watoto wangu wote, na jamaa zangu, na ambaye barua yangu itamfikia, juu ya kumcha Mwenyezi Mungu na kupangilia jambo lenu, na kuwa na uhusiano mwema kati yenu, hakika mimi nimemsikia babu yenu s.a.w.w. akisema: 'Kuboresha uhusiano kati yenu ni bora kuliko Swala na Swaumu kwa ujumla wake."**[43]

[43] Nahjul-Balaghah, barua ya 47

**Tatu:** Kuiweka hali ya siasa ya dola katika kuleta maendeleo na kukuza kiwango chake. Na hili linasisitizwa na Imam katika sira yake kwa raia na maelekezo yake kwa magavana na watumishi. Na kati ya yanayojitokeza zaidi na yanayoonekana zaidi ni mkataba wake kwa Maliki al-Ashtar wakati alipompa ugavana wa Misri. Ambapo Imam (as) anatilia mkazo katika vipengele vya mkataba huu juu ya kutekeleza uadilifu na usawa baina ya watumishi, na kuhifadhi haki zao za kimaada na za kimaanawi hata kama zitatofautiana dini zao na mielekeo yao, anasema (as):

**وَأَشْعِرْ قَلْبَكَ الرَّحْمَةَ لِلرَّعِيَّةِ، وَالْمَحَبَّةَ لَهُمْ، وَاللُّطْفَ بِهِمْ، وَلاَ تَكُونَنَّ عَلَيْهِمْ سَبُعاً ضَارِياً تَغْتَنِمُ أَكْلَهُمْ، فَإِنَّهُمْ صِنْفَانِ: إِمَّا أَخٌ لَكَ فِي الدِّينِ، وَإمّا نَظِيرٌ لَكَ فِي الْخَلْقِ،**

**"Uzoeshe moyo wako kuwa na huruma kwa raia, na upendo kwao, na kuwatendea wema. Na wala usiwe mnyama mkali mwenye madhara kwao, ukavizia fursa ya kuwang'ata (kuwatafuna), kwani wao (raia) wako wa aina mbili: Ama ni ndugu yako katika Dini au ni mfano wako katika kuumbwa (ni binadamu kama wewe)."**

Na Imam (as) anatoa angalizo kwamba jukumu lake haliishii katika kuchukua kodi kwa watu, hali ambayo sasa ni mashuhuri kwa jina la ukusanyaji wa mapato, bali hakika yeye anakusudia urekebishaji wa mambo ya watu wa mji katika pande zake mbalimbali, kidini na kidunia, na kuboresha nchi na kukabiliana na uadui wowote dhidi yake. Anasema (as):

هذَا مَا أَمَرَ بِهِ عَبْدُ اللهِ عَلِيٌّ أَمِيرُالْمُؤْمِنِينَ، مَالِكَ بْنَ الْحَارِثِ الْأَشْتَرَ فِي عَهْدِهِ إِلَيْهِ، حِينَ وَلاَّهُ مِصْرَ: جِبْايَةَ خَرَاجِهَا، وَجِهَادَ عَدُوِّهَا، وَاسْتِصْلاَحَ أَهْلِهَا، وَعِمَارَةَ بِلاَدِهَا.

**"Haya ndiyo ambayo mja wa Mwenyezi Mungu; Ali, Kiongozi wa Waumini anayomuamuru Malik ibn al-Haarith al-Ashtar katika mwongozo wake wa kumtawaza alipomfanya gavana wake Misri ili kukusanya kodi zake, na kupigana Jihadi dhidi ya maadui wake (wa Misri) na kuwafanyia mema watu wake (wa Misri) na kuiendeleza miji yake."**

Na Imam anatilia mkazo juu ya kipaumbele cha kuendeleza na kuongeza uzalishaji kwa kusema:

وَلْيَكُنْ نَظَرُكَ فِي عِمَارَةِ الْأَرْضِ أَبْلَغَ مِنْ نَظَرِكَ فِي اسْتِجْلاَبِ الْخَرَاجِ، لِأَنَّ ذلِكَ لاَ يُدْرَكُ إِلاَّ بَالْعِمَارَةِ، وَمَنْ طَلَبَ الْخَرَاجَ بِغَيْرِ عِمَارَة أَخْرَبَ الْبِلاَدَ، وَأَهْلَكَ الْعِبَادَ، وَلَمْ يَسْتَقِمْ أَمْرُهُ إِلاَّ قَلِيلاً.

**"Mazingatio yako yawe kwenye uendelezaji wa ardhi (kilimo) zaidi kuliko ukusanyaji wa kodi, kwani hilo (la kodi) halipatikani isipokuwa kwa kilimo, na mwenye kutaka mapato bila ya kulima atakuwa ameiharibu nchi, na kuwaangamiza waja, na suala lake halitokuwa imara ila kidogo."**

Na Imam (as) anazungumza katika mkataba huu kuhusu jukumu la kila tabaka kati ya matabaka ya jamii kama vile maaskari, makadhi, watumishi, watu wa viwandani, wakulima, wafanyabiashara jukumu la kila mmoja katika uendelezaji na kuleta maendeleo, kwa kupanga wajibu wa dola katika kuwasaidia wao na kuamiliana pamoja nao. Anasema (as):

وَاعْلَمْ أَنَّ الرَّعِيَّةَ طَبَقَاتٌ لاَ يَصْلُحُ بَعْضُهَا إلاَّ بِبَعْضٍ، وَلاَ غِنَى بِبَعْضِهَا عَنْ بَعْضٍ

**"Na tambua ya kwamba raia wako katika matabaka tafauti, baadhi ya matabaka hayapati ufanisi ila kwa ushirikiano na baadhi ya matabaka mengine, wala baadhi yao hayajitoshelezi bila ya mengine."**

Na anatilia mkazo juu ya kumchagua mtumishi wa dola kwa kutegemea kipaji na ujuzi na sio kwa msukumo wa uhusiano na ushawishi wa makundi. Kisha kuwepo na ufuatiliaji na usimamizi na uangalizi juu yao, ili wasizembee katika kazi zao, na wala wasitumie vibaya nafasi zao. Anasema (as):

ثُمَّ انْظُرْ فِي أُمُورِ عُمَّالِكَ، فَاسْتَعْمِلْهُمُ اخْتِبَاراً، وَلاَ تُوَلِّهِمْ مُحَابَاةً وأَثَرَةً، فَإِنَّهُمَا جِمَاعٌ مِنْ شُعَبِ الْجَوْرِ وَالْخِيَانَةِ. وَتوَخَّ مِنْهُمْ أَهْلَ التَّجْرِبَةِ وَالْحَيَاءِ، مِنْ أَهْلِ الْبُيُوتَاتِ الصَّالِحَةِ، وَالْقَدَمِ فِي الْإِسْلاَمِ الْمُتَقَدِّمَةِ، فَإِنَّهُمْ أَكْرَمُ أَخْلاَقاً،

**وَأَصَحُّ أَعْرَاضاً، وَأَقَلُّ فِي الْمَطَامِعِ إِشْرَافاً، وَأَبْلَغُ فِي عَوَاقِبِ الْأُمُورِ نَظَراً. ثُمَّ أَسْبِغْ عَلَيْهِمُ الْأَرْزَاقَ، فَإِنَّ ذٰلِكَ قُوَّةٌ لَهُمْ عَلَى اسْتِصْلاَحِ أَنْفُسِهِمْ، وَغِنىً لَهُمْ عَنْ تَنَاوُلِ مَا تَحْتَ أَيْدِيهِمْ، وَحُجَّةٌ عَلَيْهِمْ إِنْ خَالَفُوا أَمْرَكَ أَوْ ثَلَمُوا أَمَانَتَكَ.ثُمَّ تَفَقَّدْ أَعْمَالَهُمْ، وَابْعَثِ الْعُيُونَ مِنْ أَهْلِ الصِّدْقِ وَالوَفَاءِ عَلَيْهِمْ، فَإِنَّ تَعَاهُدَكَ فِي السِّرِّ لِأُمُورِهِمْ حَدْوَةٌ لَهُمْ عَلَى اسْتِعْمَالِ الْأَمَانَةِ، وَالرِّفْقِ بِالرَّعِيَّةِ.**

**"Kisha angalia mambo ya wafanyakazi wako, wape kazi baada ya majaribio, usiwachague kwa upendeleo au ufadhili, kwani viwili hivi ni mkusanyiko wa matawi ya dhulma na khiyana. Wachague katika wao wenye uzoefu na adabu, kutoka katika watu wa nyumba njema, na waliotangulia katika Uislamu, kwani wao wana tabia njema sana, na asili sahihi, na wenye muelemeo mdogo wa tamaa. Wana mtizamo yakini wa matokeo ya mambo. Kisha wakamilishie riziki ya wasaa (mshahara mkubwa), kwani hilo huwa ni nguvu kwa ajili ya kujiweka vyema wao wenyewe, na wao kutosheka na kutogusa kilicho chini ya uangalizi wao. Na ni hoja dhidi yao endapo watakhalifu amri yako, au kuitia dosari amana yako. Kisha chunguza kazi zao, tuma waangalizi miongoni mwa watu wa kweli na watekelezaji juu yao, kwa kuwa kuwafuatilia kwako kwa siri mambo yao, ni msukumo kwao wa kuwa waaminifu, na kuwa wapole kwa raia."**

Kama ambavyo Imam anaelekeza dola kwenye kuwajali mafakiri, wenye haja na wenye maradhi sugu, na kwamba ni wajibu wake kutafuta sehemu za udhaifu na haja katika jamii, na katika kuwaangalia wao dola itegemee wenye uaminifu na muamala mzuri. Anasema (as):

ثُمَّ اللهَ اللهَ فِي الطَّبَقَةِ السُّفْلَى مِنَ الَّذِينَ لاَ حِيلَةَ لَهُمْ وَالْمَسَاكِينَ وَالْمُحْتَاجِينَ وَأَهْلِ الْبُؤْسَى وَالزَّمْنَى، فإِنَّ فِي هذِهِ الطَّبَقَةِ قَانِعاً وَمُعْتَرّاً، وَاحْفَظْ لِلَّهِ مَا اسْتَحْفَظَكَ مِنْ حَقِّهِ فِيهِمْ، وَاجْعَلْ لَهُمْ قِسماً مِنْ بَيْتِ مَالِكَ، وَقِسماً مِنْ غَلاَّتِ صَوَافِي الْإِسْلاَمِ فِي كُلِّ بَلَدٍ، فإِنَّ لِلْأَقْصَى مِنْهُمْ مِثْلَ الَّذِي لِلْأَدْنَى، وَكُلٌّ قَدِ اسْتُرْعِيتَ حَقَّهُ، فَلاَ يَشْغَلَنَّكَ عَنْهُمْ بَطَرٌ، فَإِنَّكَ لاَ تُعْذَرُ بِتَضْيِيعِ التَّافِهَ لِإِحْكَامِكَ الْكَثِيرَ الْمُهِمَّ. فَلاَ تُشْخِصْ هَمَّكَ عَنْهُمْ، وَلاَ تُصَعِّرْ خَدَّكَ لَهُمْ، وَتَفَقَّدْ أُمُورَ مَنْ لاَ يَصِلُ إِلَيْكَ مِنْهُمْ مِمَّنْ تَقْتَحِمُهُ الْعُيُونُ، وَتَحْقِرُهُ الرِّجَالُ، فَفَرِّغْ لِأُولئِكَ ثِقَتَكَ مِنْ أَهْلِ الْخَشْيَةِ وَالتَّوَاضُعِ، فَلْيَرْفَعْ إِلَيْكَ أُمُورَهُمْ،

**“Kisha tahadhari sana juu ya watu wa tabaka la chini, miongoni mwao ambao hawana hila, na masikini na wahitaji, na ambao ni hohehahe na wenye ulemavu, kwani katika tabaka hili kuna anayeomba na asiyetosheka. Na hifadhi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu wajibu Wake miongoni mwa haki Yake kwao. Na wajaalie sehemu kutoka mfuko wa hazina ya mali yako, na sehemu kutokana na mazao ya ardhi ya ngawira ya Kiislam katika kila mji, kwani aliye mbali miongoni mwao ni sawa na aliye karibu, na wote kila mmoja haki yake imewekwa chini ya uangalizi wako. Hivyo basi asikushughulishe kutokana nao yule mkorofi, kwa kweli wewe hutopewa udhuru kwa kupoteza jambo hafifu, eti kwa sababu ya kutilia maanani mengi yaliyo muhimu. Kwa hivyo usiiondoe hima yako mbali nao, wala usiwatazame watu kwa upande mmoja wa uso wako (usiwafanyie jeuri). Na yaangaliye mambo ya wale ambao hawawezi kuwasiliana na wewe miongoni mwao kati ya wale ambao macho yanadharau kuwaona, na watu kuwadharau, basi teuwa watu unaowaamini wakae nao faragha ili kujua hali zao, watu hao (wa kukaa nao) wawe miongoni mwa wachamungu na wanyenyekevu, hao wakufikishie mambo yao.»**

Hakika waraka wa Imam Ali kwa Maliki al-Ashtari unatengeneza waraka wa kisiasa mzuri wa kimalezi, na wala haipasi tuusome kwa kuuzingatia kuwa ni njia ya mtawala tu, bali ni wajibu wetu tujifunze kwa mtazamo wa kwamba unawakilisha jukumu la jamii katika kufanikisha uendelezaji wa jumla wa jamii.

**Jamii zetu na Dharura ya Uendelezwaji:**

Kuna tofauti kubwa na upeo mpana baina ya mahitaji yanayotimizwa na nchi zilizoendelea kwa raia wake, ikiwa ni pamoja na mazingira ya maisha mazuri, fursa ya kusoma, kazi ya uzalishaji, huduma ya afya, mazingira ya uhuru na demokrasia, na baina ya hali ya nchi zinazoendelea, ambapo katika nchi hizi kuna hali ya kutoendelea na sehemu kubwa ya raia haina kiwango kinachokubalika kiakili cha maisha mazuri, kwa sababu ya ufakiri, kuenea hali ya kutojua kusoma, ukosefu wa fursa ya kusoma na kazi, sambamba na ukosefu wa uhuru, na kushamiri ukandamizaji wa kifikra na kisiasa.

Na tofauti hii imepelekea mamilioni ya vijana wa nchi zinazoendelea au za ulimwengu wa watatu, kutafuta kila njia na fursa yoyote ya kuhama na kukimbilia kufanya kazi katika nchi zilizoendelea. Na unatosha mfano juu ya hilo yale tunayoyaona kati ya matukio yenye kuhilikisha na yenye kujirudia rudia ambayo yanawakabili maelfu ya vijana wa Kiafrika na sehemu za Kiarabu, kwa kuhatarisha roho zao na mali zao kwa uhamiaji haramu kupitia bahari, katika mazingira yasiyo salama na yasiyo na dhamana, na kwenda nchi zilizoendelea za Ulaya ya Magharibi na Australia, na baadhi yao kuishia kuwa ni chakula cha samaki baharini. Ukiachilia safu ndefu za kuomba viza ya kuhamia au kazi katika balozi za kigeni katika nchi zetu za Kiarabu.

Na tunakuta kwa mfano matajiri na wenye rasilimali kubwa wanapotaka uzalishaji wenye uhakika wenye faida nzuri, hakika wao wanawekeza na kuzalisha mali zao huko, na kwa sababu hii mabilioni ya dola za Waarabu zinachukua njia zake za uwekezaji na uzalishaji katika nchi za Ulaya na Marekani, kwa nini? Kwa sababu nchi hizo zina mazingira mazuri kwa ajili ya uzalishaji wa kiuchumi na tija, na mazingira ya kazi ni mazuri na ni yenye usalama wa kisheria. Na hapa ndipo inapojitokeza tamaa hii kubwa, na tofauti ni kubwa baina ya nchi hizo na nchi za ulimwengu wa tatu.

Na kutokana na taasisi za kimataifa kujua hatari ya jambo hili, Umoja wa Mataifa umeanzisha kitengo chini ya anwani ya 'Mpango wa Maendeleo' unaojali mambo ya kuendeleza binadamu, na kitengo kinatoa kila mwaka ripoti ya kimataifa juu ya Maendeleo ya Binadamu katika nchi mbalimbali za ulimwengu, na katika mpango huu zimetolewa hadi sasa ripoti nne hususan kuhusu nchi za Kiarabu chini ya anwani ya 'Ripoti ya Maendelelo ya Binadamu Katika nchi za Kiarabu.'

Na baada ya kuafikiwa mwelekeo huu, baadhi ya nchi za Kiarabu zimetoa ripoti yake maalumu ya ndani inayohusu maendeleo. Katika nchi ya Saudia tangu mwaka 2003 Wizara ya Uchumi na Mipango imekuwa inatoa ripoti kila mwaka inayofuatilia hali ya maendeleo katika nchi.

Wataalamu wametambulisha Maendeleo ya Binadamu - kama ilivyokuja katika Ripoti ya Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Uendelezaji wa mwaka 1990 – kwamba ni kuongezeka na kukua wigo wa kutoa mahitaji kwa watu. Na mahitaji hayo yanaweza kuwa ni yenye kubadilika kulingana na wakati na yasiyokuwa na mwisho, isipokuwa katika viwango vyote vya maendeleo, mahitaji ya aina tatu ya lazima ambayo ni wajibu yapatikane ni: Kuwa na maisha ma-

zuri ya kiafya na ya muda mrefu, kupata maarifa, na kupata mahitaji ya lazima kwa ajili ya kupata maisha mazuri.

Katika kumwendeleza mwanadamu kuna pande mbili:

**Kwanza:** Ni kutengeneza uwezo wa kibinadamu, mfano kuboresha kiwango cha afya na cha maarifa na kuendeleza vipaji.

**Pili:** Ni watu kunufaika kutokana na vipaji hivi vya kujifunza katika kazi za uzalishaji, harakati za kijamii, kisiasa na shughuli za kiutamaduni.

Wakati ambapo tunapokuta kuna hali ya kutokuendelea na kwamba kuna sehemu zenye mapungufu katika nyanja za maisha ambazo ni wajibu ziwe kamili kwetu kama wanadamu na kama raia, hakika ni juu yetu tufikiri katika kuboresha hali zetu na mazingira yetu. Na swali hapa ni kwamba ni nani mwenye kuwajibika katika kufanikisha na kuleta maendeleo ya binadamu? Watu wengi wanaitakidi kwamba anayepasa kuwajibika ni serikali ambayo mikononi mwake mna mamlaka ya kutawala pato la nchi na ndiyo inayolengwa moja kwa moja katika kumwendeleza binadamu katika jamii. Na hii ni sahihi kwa kiasi kikubwa, serikali zinabeba wajibu wa msingi na mkubwa katika mas'ala haya, lakini haiwezekani kusahau wajibu wa jamii na raia katika kuihimiza serikali kwa ajili ya kuweka siasa ya uendelezaji sahihi, na kwa ajili ya utekelezaji sahihi na bora kupitia harakati zake na shughuli zake na pato lake, na kwa sababu hiyo ripoti zimeashiria kwenye umuhimu wa jukumu la vyama vya kiraia vya kijamii na asasi za kiraia katika mwelekeo huu.

Na hapa haisihi kuelekeza lawama juu ya serikali tu, na kuzingatia kuwa nafsi zetu ziko kando katika kubeba jukumu na wajibu huu, na hatimaye kuishia kutoa malalamiko kwa madai kwamba serikali haikushughulika na kufanya kitu kinachotakiwa. - Na swali muhimu ni: Ni upi wajibu wa raia? Na kwa kujibu swali hili, kuna mambo

matatu ni wajibu tuyafikirie na tuyazingatie kwa ajili ya kuzisaidia nafsi zetu na kuboresha hali zetu na kuinua kiwango cha jamii yetu.

**Uzalishaji na Kusambaza Utamaduni wa Maendeleo:**

Kama ambavyo maendeleo yana utamaduni wake, vile vile uzembe na uvivu vina utamaduni wake, na huenda tatizo letu linatokana na kuenea na kusambaa aina ya pili ya utamaduni katika mazingira yetu. Sisi tuna haja ya utamaduni hai unaomsukuma kila mmoja wetu katika kuibua uwezo wake na kufanya kazi kwa kadiri ya uwezo wake kwa ajili ya kuboresha hali yake binafsi, na kusaidia katika kuboresha hali za wengine.

Na huenda moja ya matatizo ya ajabu sana ni pale tunapokuta baadhi yetu hawajali kabisa wala hawafanyi juhudi yoyote ya kubeba jukumu kwa ajili ya nafsi yake, ukiachilia mbali kujitahidi na kujituma kubeba jukumu kwa ajili ya watu wengine. Utakuta mmoja kati ya hawa anaishi katika ufakiri na anakubaliana nao na anaishi kwa uzembe na ananyenyekea katika uzembe huo, na anaishi katika ujahili na wala hafanyi juhudi ya kuendelea na masomo na kupata maarifa.

Na lililo baya zaidi katika utamaduni wa uzembe ni kudhihirisha baadhi ya sehemu za utamaduni wa kidini ili kuengua na kuficha ukweli ili hatimaye dini iwe inatumikia hali ya uzembe na uvivu, na hiyo ni kwa njia ya watu kuyapa nyongo maisha ya dunia. Wameghafilika kwamba dunia hii ndio chumo la Akhera, na kwamba yeyote ambaye ni mwenye kushindwa katika dunia yake basi ni mwenye kushindwa zaidi katika Akhera yake. Na kwamba asiye na maisha basi hana marejeo, kama lilivyo tamko na madhumuni ya riwaya nyingi. Na ndani ya mazingira ya utamaduni huu wa uzembe tunakutana na aina ya watu wasiokuwa na lengo isipokuwa kudhoofisha azma, wao wa-

nakufanya usiwe na hisia ya kujali kazi yoyote unayotaka kuifanya, ukitaka kufanya mradi wa kiuchumi wanakuhofisha kuwa utapata hasara, na ukifikiria kwenda kufanya kazi sehemu nyingine yoyote mbali na mji wako wanapanda kwako hofu ya ugeni, na unapotaka kushirikiana na wengine katika shughuli wanakuhadharisha na ushirikiano mbaya wa wengine, na ni hivyo ndivyo walivyo na aina za utamaduni mbaya wa kudhoofisha azma.

Kuanzia hapa sisi tuna haja ya utamaduni ambao unafungua mbele ya watu upeo wa matarajio na uoni katika maisha haya, na ambao unaondoa mbele yao vikwazo vinavyozuia kufanya kazi. Na inapasa kwa makhatibu wa kidini na taasisi za kidini na vyombo vya habari kutilia mkazo utamaduni wa maendeleo na uzalishaji, matarajio, na raghaba ya kupenda maendeleo kwa njia ya kujituma na kufanya kazi.

**Kazi ya Raia na Taasisi za Kiraia:**

Ripoti zilizotolewa na Taasisi za Kimataifa na Umoja wa Mataifa zinatilia mkazo juu ya umuhimu wa jukumu la vyama vya kijamii na asasi za kiraia. Hiyo ni kwa sababu uwepo wa asasi za kiraia unatoa ishara juu ya maendeleo ya kiwango cha uelewa kwa watu, kama ambavyo zinaashiria kwamba watu wanabeba jukumu la nafsi zao na ufaulu wao katika kutengeneza hali ya ushirikiano baina yao, na jambo hili lina umuhimu sana katika jamii yoyote. Nchi zilizoendelea zinalalamikia wingi wa asasi za kiraia na vyama vya kijamii, ambapo inakaribia kutopata sekta yoyote ya kimaisha isipokuwa ina asasi ya kiraia inayojishughulisha na sekta hiyo au taasisi ya kijamii inayofuatilia jambo hilo. Watu hao katika kujali kwao ubinadamu wameshavuka mipaka ya nchi zao, na hivyo wameanzisha vyama vya kiraia ambavyo vinafanya kazi zake katika kiwango cha ulim-

wengu, kuna asasi za haki, tiba na misaada, taasisi ya Kimataifa ya Haki za Binadamu, au matabibu wasio na mipaka, au Jumuiya ya Kimataifa ya kutoa misaada, hizi zimekuwa mashuhuri mno hazihitaji kutambulishwa.

Hadi mwanamke mmoja kama vile mama Theresa (aliyezaliwa mwaka 1910 na kufariki mwaka 1997) anayetoka Macedonia katikati ya Ulaya anajishughulisha na kazi ya kibinadamu katika mafunzo yake ya kuhubiri Injili India na Afrika, na ameanzisha kupitia harakati zake za maisha maelfu ya mahema na makazi ya wakimbizi, na kupokea maelfu ya mayatima, wagonjwa, wasiojiweza na wenye maradhi yasiyopona. Na kwa masikitiko makubwa mukabala na hayo tunakuta baadhi ya jamii zetu hazifanyi juhudi yoyote ya kutatua haja zake ndani katika mji na kijiji, na hakika baadhi ya hali ambazo zinaishi nayo jumuiya za kujitolea na vituo vya misaada katika maeneo yetu ni za aibu. Ukitazama baadhi ya ripoti zilizotolewa kutoka katika jumuiya hizi zinafichua kwamba kiwango cha misaada inayokuja kutoka nje ya maeneo yake ni maradufu ya ile ambayo inayokuja kutoka ndani.

Na huenda haja ya kuwa na asasi kama hizi haitokani tu na haja ya kutatua mahitaji ya jamii tu, bali pia kwa ajili ya kufuatailia na kuwasiliana na idara za serikali. Na hapa ndipo unapojitokeza umuhimu wa fikra iliyotolewa ambayo inatumiwa na Halmashauri za Miji katika kuanzisha kile kinachoitwa Mabaraza ya Kata. Na umuhimu wake ni kuleta uzingativu kwa watu wa kila kata kuona dharura ya kujali na kutilia umuhimu mambo ya kata yao wanayoishi kupitia uzoefu wao wa kuchagua kundi la wajumbe watakaoendesha baraza hili, na kuelekeza juhudi zake katika kutekeleza mahitaji ya kata katika huduma mbalimbali kwa kushirikiana na pande husika.

**Mipango ya Maendeleo:**

Sisi tuna haja ya kuwa na kamati za kiraia zaidi ya hizi tulizonazo na kuvuka orodha tuliyonayo sasa. Na kuna haja ya kuwa na kamati nyingi zinazo shughulikia mpango wa kusaidia mafunzo ya jumla, na juhudi za wananchi zinazofuatilia shule za mafunzo na kuamilana nazo. Na kwa namna hiyo hiyo tuna haja sana ya kuwa na kamati za raia zenye kusaidia sekta ya afya, na huenda kamati ya marafiki wa wagonjwa iliyo chini ya kitengo cha biashara cha Mkoa wa Mashariki ni mfano bora. Ni kwa nini hatuundi kamati ya marafiki wa wagonjwa katika eneo letu kwa lengo la kutembelea hizi hospitali na kuwasiliana na idara zake kwa ajili ya kuziba baadhi ya mapungufu na kuwasilisha malalamiko na mapendekezo sehemu husika? Hii kwa hakika itaifanya idara ya hospitali kuwa na jitihada zaidi na azma katika kushirikiana na kushughulikia matatizo, makosa mbalimbali na mapungufu yaliyopo.

Wagonjwa wengi katika nchi yetu wanawaendea wafadhili kwa lengo la kutaka msaada wa matibabu au kwa ajili ya kushindwa kwao kununua dawa, na haya ni mambo ambayo yanatutaka tuunde vitengo vya kijamii vinavyowaangalia watu mfano wa hawa. Na yanajirudia mambo vilevile katika upande wa kazi, na hapa ni muhimu kuelezea juhudi za kitabibu mbele ya baadhi ya jumuiya za kujitolea ambazo zimejitolea kuanzisha vitengo vya kuwezesha kufanya kazi na kusaidia vijana katika kupata nafasi za kazi. Na sisi tunakumbuka kuhusiana na maudhui haya sanduku la mia mia ambalo fikra yake ya msingi imetokana na kiongozi wa kiingereza Prince Tashalis, na ambaye lengo lake la msingi linalenga katika kuwasukuma vijana katika kupata na kuanzisha miradi na taasisi ndogo ndogo kwa kutegemea msaada wa sanduku hili, na kutoa ujuzi na wepesi wa maisha. Sanduku hili limefungua njia yake kidogo kidogo katika maeneo mbalimbali ulimwenguni, na kwa hakika kutokana

na lengo hilo, sanduku la mia mia limeanzishwa katika nchi yetu ya Saudia kabla ya miaka miwili takriban.

Na mambo ni vivyo hivyo katika kiwango cha utamaduni. Sisi tuna haja ya kujitolea kwa ajili ya vijana wetu katika kiwango cha teknolojia na utamaduni unaojali kazi za kujitolea katika nyanja mbalimbali. Na kwa uongofu huu mambo yatakuwa katika kilele cha tabia njema ya kimaendeleo, kama atajitolea baina yetu ambaye yuko tayari kujishughulisha na uzalishaji wa kiutamaduni kwa waandishi wasioweza kuchapisha kazi zao za kiutamaduni, kifasihi na kidini.

# NDIO, KWA KUANZISHA VYAMA VYA KIRAIA

## VYA KIJAMII KATIKA NCHI YETU[44]

Sheikh Hasan Safar amelingania juu ya harakati za kijamii na kiutamaduni, na kuwataka wananchi wa Saudia kujitolea kwa kuanzisha taasisi na vyama vya kijamii vya kiraia ambavyo amevielezea kwamba vinaweza kujenga na kutumia vipaji, kuratibu na kuendeleza mambo yetu mbalimbli ya kimaisha. Sheikh Safar amesema katika muhadhara wake wa kuhitimisha ratiba ya "Ali na Ummah" usiku uliopita, ikiwa ni mnasaba wa kumbukumbu ya kifo cha kishahidi cha Imam Ali (as), kwamba kazi ya raia hata kama itakuwa haizidi utekelezaji wa serikali lakini pia haipungui umuhimu katika upande wa kuiendeleza jamii. Ameihutubia hadhira ambayo ilijaa uwanja wa Shawikah huko Qatif, kwamba harakati za wananchi ndio mpangaji wa kimsingi na mwendeshaji moja kwa moja wa kazi ya serikali. Kwa kuongezea kwamba haijuzu kuiachia jukumu lote serikali na wanajamii kujivua wajibu wa kuendeleza na kuboresha hali zao za kimaisha.

Sheikh Safar ameashiria kwamba uendelezaji wa kijamii una haja ya mambo matatu muhimu: La kwanza ni kusambaza na kueneza utamaduni wa maendeleo na kuwajibika mkabala na utamaduni wa uzembe na uvivu.  Na la pili ni kuunga mkono kazi ya wananchi na taasisi za kiraia.  Na la tatu ni kuwepo mpango wa maendeleo katika upande wa mafunzo, afya na kazi. Na ameongeza kwamba

[44] Imesambazwa katika tovuti ya Raswidi al- ikhibariya tarehe 13/ 10/ 2006

sisi tuna haja ya kuwa na utamaduni unaowasukuma watu kwenye uelewa na matarajio, na unaosukuma kwenye mwelekeo wa kusaidi-ana na kujituma, na sio uzembe na kudumaa. Kama ambavyo ame-ona kwamba kuanzisha vyama vya kiraia vya kijamii katika sehemu yoyote ni dalili njema na inaashiria kuendelea kwa utamaduni wa kushirikiana na kazi ya pamoja. Na amewalingania wote katika ku-jitolea kuanzisha vyama vya kiraia katika sekta mbalimbali katika kuhudumia jamii.

Sheikh Safar ameashiria kwamba jamii yetu katika njia ya mwamko ina haja ya kuwa na makumi ya vyama vya kiraia katika sekta mbalimbali za mafunzo, kujali wenye vipaji, kusaidia mafunzo ya juu, kuangalia wagonjwa, kutafutia ajira wasio na kazi na kusaid-ia miradi maalum na kazi katika nchi. Pia amekosoa sana mwele-keo wa wanajamii wengi kujiingiza katika kazi katika mashirika na wakati mwingine kwa malipo madogo na duni chini ya visingizio visivyokinaisha, badala ya kuanzisha kazi na miradi maalum na mi-kubwa.

Sheikh Safar mwishoni mwa muhadhara wake ametoa wito wa kumwiga Imam Ali (as) ambaye aliweza katika muda mchache wa utawala wake uliojaa mkanganyiko na fitina kumaliza ufakiri na umaskini, na kuleta uadilifu katika jamii ya Kiislamu, kuleta uhuru wa kutoa mawazo na maoni kwa watu wote wakiwemo wapinzani wake.

## MAONYESHO YA VITABU YA QATIF:

Sambamba na ratiba ya (Ali na Ummah) kamati ya usimamizi ili-panga kwa muda wa siku tatu maonyesho ya vitabu ya Qatif yaliyo-husisha zaidi ya anwani za waandishi 1200 wanaume na wanawake

miongoni mwa wananchi wa mkoa wa Qatif. Maonyesho ambayo yalifanyika katika uwanja wa Shawikah yamevutia kwa muda wa siku tatu mamia ya wasomi na watembeleaji na wanaopenda kusoma. Amesema Ustadh Amin Taruwatiy mkuu wa kamati ya Imam Hasan (as) kwamba mpango wa maonyesho umekuja kwa heshima ya waandishi wa ndani na kudhihirisha kiwango cha utajiri wa utamaduni wa sehemu hii. Tarutiy aliashiria kwamba kuna makumi mengine ya anwani ambazo hazikupata fursa ya kuonyeshwa kutokana na sababu mbalimbali, alitamani kupata fursa nyingine ya kufanya maonyesho yanayofanana na hayo katika siku za usoni.

# ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA

## AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa

17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.

39 Upendo katika Ukristo na Uislamu

40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili

41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu

42. Kupaka juu ya khofu

43. Kukusanya swala mbili

44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara

45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya

46. Kusujudu juu ya udongo

47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)

48. Tarawehe

49. Malumbano baina ya Sunni na Shia

50. Kupunguza Swala safarini

51. Kufungua safarini

52. Umaasumu wa Manabii

53. Qur'an inatoa changamoto

54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm

55. Uadilifu wa Masahaba

56. Dua e Kumayl

57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu

58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake

59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata

60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)

81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usuni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
100. Idil Ghadiri
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102 Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi

103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Maarifa ya Kiislamu
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa

125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah

146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)

147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)

148. Ndugu na Jirani

149. Ushia ndani ya Usuni

150. Maswali na Majibu

151. Mafunzo ya hukmu za ibada

152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisuni No 1

153 Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisuni No 2

154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisuni No 3

155. Abu Huraira

156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.

157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza

158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili

159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza

160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili

161. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili

162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)

163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani

164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu

165. Uislamu Safi

166. Majlisi za Imam Husein Majumbani

167. Mshumaa.
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu
(Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Jihadi ya Imam Hussein ('as)
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi

188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Mwonekano wa Upotoshaji katika Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina (‘as) na Makhalifa
197. Uongozi na Utawala katika Mwenendo wa Imam ‘Ali (‘a)
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu na vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni wa Kisunni na Mwanachuoni wa Kishia (*Al- Muraja’aat*)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Upotoshaji dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)

209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza
213. Imam Ali na Mambo ya Umma

# KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba'Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi